# KATIBA YA ZANZIBAR YA 1984

## Toleo la 2020

(Toleo hili la Katiba ya Zanzibar ya 1984 linajumuisha na kuweka pamoja marekebisho yote ya Katiba ya Zanzibar yaliyofanywa kuanzia mwaka 1985 hadi mwaka 2016 kwa madhumuni ya kurahisisha marejeo ya Katiba)

Zanzibar
17 Agosti, 2020

{ SAID H. SAID }
Mwanasheria Mkuu
Zanzibar

# KATIBA YA ZANZIBAR

## SURA YA KWANZA

### Zanzibar na Watu

### Sehemu ya Kwanza
### Zanzibar

1. Zanzibar na mipaka yake.
2. Zanzibar na Muungano.
2A. Mikoa na Wilaya za Zanzibar.
3. Muhuri wa Serikali na alama nyenginezo.
4. Katiba ya Zanzibar.
5. Zanzibar kufuata mfumo wa vyama vingi.
5A. Mgawanyo wa madaraka.

### Sehemu ya Pili
### Watu

6. Mzanzibari.
7. Haki ya kupiga Kura.

## SURA YA PILI

### Malengo na Maamuru Muhimu ya Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

8. Wajibu mkubwa wa Serikali.
9. Serikali na Watu.
10. Malengo ya kisiasa.
10A. Mabadilliko ya masharti ya Sura ya Pili.

## SURA YA TATU

## Kinga ya Haki za Lazima, Wajibu na Uhuru wa Mtu Binafsi

11. Usawa wa Binaadamu.
12. Usawa mbele ya Sheria.
13. Haki ya kuwa hai.
14. Haki ya uhuru wa mtu binafsi.
15. Haki ya faragha ya mtu na usalama wake.
16. Kinga ya uhuru wa kwenda.
17. Kinga kutokana na kudhulumiwa mali.
18. Uhuru wa maoni.
19. Uhuru wa mtu kuamini dini atakayo.
20. Kinga kwa uhuru wa kujikusanya na kujiunga.
21. Uhuru wa kushiriki shughuli za umma, haki ya kufanya kazi na kupata ujira.
22. Wajibu wa kushiriki kazini.
23. Wajibu wa kutii sheria za nchi, kulinda mali ya umma na ulinzi wa Taifa.
24. Mipaka kwa haki na uhuru, na hifadhi kwa haki na wajibu wake.
25. Haki za lazima na uhuru wa binafsi.
25A. Kufungua mashauri.

## SURA YA NNE

## Serikali

### Sehemu ya Kwanza

### Rais

26. Afisi ya Rais na sifa za kuchaguliwa kuwa Rais.
27. Uchaguzi wa Rais.
28. Muda wa kuendelea na Urais.

29. Kuongezwa kwa kipindi cha miaka mitano.
30. Kutofaa kuwa Rais.
31. Kiapo cha Rais.
32. Kuachishwa Urais kwa ugonjwa.
33. Nafasi katika kiti cha Urais.
34. Mpango wa uchaguzi iwapo kiti cha Rais kiwazi.
35. Mshahara na malipo mengine ya Rais.
36. Rais hatashtakiwa akiwa kazini.
37. Baraza la Wawakilishi laweza kumshtaki Rais.
38. Hadhi ya Rais aliyepita.

**Sehemu ya Pili**

**Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais**

39. Makamo wawili wa Rais.
39A. Kuachwa wazi kwa nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.
40. Kuwa wazi kwa nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais.
41. Hoja ya kura ya kutokuwa na imani.

**Sehemu ya Tatu**

**Mawaziri, Naibu Mawaziri na Baraza la Mapinduzi**

42. Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
42A. Kuacha kufanyakazi kwa Makamo wa Kwanza na Mawaziri.
43. Baraza la Mapinduzi.
44. Ugawaji wa Wizara kwa Mawaziri
45. Mikutano ya Baraza.
46. Viapo vya uaminifu.
47. Naibu Mawaziri.
48. Nafasi ya Waziri, Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi kuwa wazi.
49. Katibu wa Baraza la Mapinduzi.
50. Katibu Mkuu.

**Sehemu ya Nne**

**Madaraka ya Serikali**

51. Malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
52. Kutolazimika kwa Rais kufuata ushauri wa mtu.
53. Uanzishaji wa Afisi na Wadhamini wa Afisi hizo.
54. Muda wa kufanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
55. Mwanasheria Mkuu.
56. Kazi za Mwanasheria Mkuu.
56A. Mkurugenzi wa Mashtaka.
57. Kiapo cha uaminifu.
58. Washauri Maalum.
59. Uwezo wa kutoa msamaha.
60. Kamati ya Ushauri katika uwezo wa kutoa msamaha.
61. Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.
62. Kazi za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

**SURA YA TANO**

**Baraza la  Wawakilishi**

**Sehemu ya Kwanza**
**Muundo wa Baraza la Kutunga Sheria**

63. Baraza la Kutunga Sheria.
64. Kuanzishwa kwa Baraza Ia Wawakilishi.
65. Uchaguzi wa Wajumbe wa kuchaguliwa.
66. Wajumbe wa kuteuliwa.
67. Wajumbe Wanawake katika Baraza.
68. Sifa za kuchaguliwa.
69. Kutofaa kuchaguliwa.
70. Kiapo cha Mjumbe Mwakilishi.

71. Muda wa Wajumbe kushika madaraka yao.
72. Uamuzi wa suala kama mtu ni mjumbe Mwakilishi ama sio.
73. Spika.
74. Naibu Spika.
75. Taratibu za uchaguzi wa Spika na Naibu Spika.
76. Katibu wa Baraza la Wawakilishi.
77. Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

**Sehemu ya Pili**
**Sheria na Taratibu Katika Baraza la Wawakilishi**

78. Nguvu za kutunga Sheria.
79. Utaratibu wa kutunga Sheria.
80. Kubadilisha Katiba.
80A. Kura ya maoni kwa mabadiliko ya baadhi ya vifungu vya Katiba.
81. Uongozi wa kikao cha Baraza la Wawakilishi.
82. Viti vilivyo wazi katika Baraza la Wawakilishi na utaratibu wa kuendesha shughuli za Baraza.
83. Upigaji kura katika Baraza la Wawakilishi.
84. Madaraka ya Rais katika Baraza la Wawakilishi.
85. Kamati za Baraza la Wawakilishi
86. Baraza kutunga Sheria.
87. Lugha rasmi.
88. Kazi za Baraza la Wawakilishi.

**Sehemu ya Tatu**
**Kuitisha na Kuvunja Baraza la Wawakilishi**

89. Kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi
90. Uchaguzi Mkuu na Mkutano wa mwanzo.
91. Kuitisha na kuvunja Baraza la Wawakilishi.
92. Maisha ya Baraza la Wawakilishi.

## SURA YA SITA

## Sheria

### Sehemu ya Kwanza

### Mahkama Kuu

93. Kuundwa kwa Mahkama Kuu.
94. Uteuzi wa Majaji wa Mahkama Kuu.
95. Muda wa kushika madaraka ya Ujaji.
96. Viapo kwa Majaji wa Mahkama Kuu.
97. Uanachama katika vyama vya siasa.

### Sehemu ya Pili

### Mahkama ya Rufaa

98. [Kimefutwa].
99. Kazi na uwezo wa Mahkama ya Rufaa.
99A. Ufafanuzi wa Katiba kupelekwa Mahkama Kuu.

### Sehemu ya Tatu

### Mahkama Nyenginezo

100. Kuanzishwa kwa Mahkama nyengine.

### Sehemu ya Nne

### Utaratibu wa kupeleka Hati na kutekeleza maagizo yaliyomokatika Hati zilizotolewa na Mahkama

101. Utekelezaji wa maagizo ya Mahkama utafanywa nchini Tanzania kote.
102. Tume ya Utumishi ya Mahkama.
102A. [Kimefutwa].
103. [Kimefutwa].

## SURA YA SABA

### Sehemu ya Kwanza

### Fedha

### Masharti ya Fedha Yahusuyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

104. Mfuko Mkuu wa Hazina na fedha nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
105. Makadirio.
106. Ruhusa ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina kwa Sheria ya Matumizi ya Fedha.
107. Malipo kwa idhini ya Hati Maalum.
108. Matumizi ya mfuko wa dharura.
109. Matumizi ya fedha kabla ya sheria kuanza kutumika.
110. Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
111. Malipo ya baadhi ya maafisa.
112. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
113. Kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### Sehemu ya Pili

### Masharti ya Fedha Yahusuyo Mambo ya Muungano.

114. Mchango wa Muungano.
115. Uwezo wa kutumia kasma.

## SURA YA NANE

### Kamisheni ya Utumishi wa Umma

116. Kamisheni ya Utumishi wa Umma.
117. Tume ya Utumishi ya Serikali.
118. Uwezo wa Tume za Utumishi.

## SURA YA TISA

### Tume ya Uchaguzi

119. Tume ya Uchaguzi.
120. Majimbo.

## SURA YA KUMI

### Idara Maalum

121. ldara Maalum.
122. Tume ya Utumishi ya Idara Maalum.
123. Uwezo wa Rais katika Idara Maalum.

## SURA YA KUMI NA MOJA

### Mamlaka ya Baadhi ya Vyombo vya Muungano

124. Mamlaka ya baadhi ya vyombo vya Muungano kutumika Zanzibar.

## SURA YA KUMI NA MBILI

## Vyombo Vyengine vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

### Sehemu ya Kwanza

### Tume ya Mipango

125. Tume ya Mipango.
126. Wajumbe wa Tume.
127. Katibu wa Tume ya Mipango.

### Sehemu ya Pili

### Serikali za Mitaa

128. Serikali za Mitaa.

## SURA YA KUMI NA TATU

### Mambo ya Jumla

129. Kujiuzulu.
130. Uteuzi mpya na kuarifiwa kuachishwa kazi.
131. Maelezo kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika Utumishi wa Serikali.
132. Sheria za Muungano.
133. Masharti ya kutoza kodi.
134. Ufafanuzi.
134A. Kufutwa Katiba ya 1979.
135. Jina la Katiba na tarehe ya kuanza kutumika.

# KATIBA YA ZANZIBAR

## UTANGULIZI

## AZIMIO LA BARAZA LA WAWAKILISHI KUWEKA KATIBA YA ZANZIBAR

**KWA KUWA** Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa tarehe 9 Oktoba, 1984 kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar ulielewa na kukubali kwamba jukumu letu katika historia ya Watu wa Zanzibar kuimarisha Umoja, kuendeleza Mapinduzi ya Kijamaa katika Zanzibar na kusukuma Mapambano ya Ukombozi na harakati za Mapinduzi nchini, katika Afrika na duniani kote;

**NA KWA KUWA** tunatambua kwamba Umoja wa Wananchi wa Zanzibar unatokana na ushirikiano wa miaka mingi tangu wakati wa mapambano ya kupigania Uhuru hadi kufikia daraja hii ya mafanikio, na unatokana na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea;

**NA KWA KUWA** tunazingatia na kuthamini kazi nzuri ya Kimapinduzi iliyofanywa na Viongozi wa Mapinduzi, wakiongozwa na Mwasisi wa Chama cha ASP na Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ambaye fikra zake zitaendelezwa na kudumishwa daima, kizazi baada ya kizazi katika kupambana na Ukoloni, Ubepari, Unyonge, Uonevu na Dharau, na badala yake kudumisha Uhuru na Umoja, Haki na Usawa, Heshima na Utu;

**NA KWA KUWA** tunatambua kwamba mafundisho na mawazo ya Kimapinduzi yatalindwa, yataendelezwa na kudumishwa kwa misingi ya Kidemokrasia;

**NA KWA KUWA** tunatambua kuwa mapambano ya kujenga Ujamaa katika Zanzibar na kushiriki kwetu kikamilifu katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar kunahitaji SHERIA madhubuti itakayowaongoza watu Ki Katiba, kutokana na fikra za Wafanyakazi na Wakulima;

# KATIBA YA ZANZIBAR

## UTANGULIZI

## AZIMIO LA BARAZA LA WAWAKILISHI KUWEKA KATIBA YA ZANZIBAR

**KWA KUWA** Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa tarehe 9 Oktoba, 1984 kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar ulielewa na kukubali kwamba jukumu letu katika historia ya Watu wa Zanzibar kuimarisha Umoja, kuendeleza Mapinduzi ya Kijamaa katika Zanzibar na kusukuma Mapambano ya Ukombozi na harakati za Mapinduzi nchini, katika Afrika na duniani kote;

**NA KWA KUWA** tunatambua kwamba Umoja wa Wananchi wa Zanzibar unatokana na ushirikiano wa miaka mingi tangu wakati wa mapambano ya kupigania Uhuru hadi kufikia daraja hii ya mafanikio, na unatokana na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea;

**NA KWA KUWA** tunazingatia na kuthamini kazi nzuri ya Kimapinduzi iliyofanywa na Viongozi wa Mapinduzi, wakiongozwa na Mwasisi wa Chama cha ASP na Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ambaye fikra zake zitaendelezwa na kudumishwa daima, kizazi baada ya kizazi katika kupambana na Ukoloni, Ubepari, Unyonge, Uonevu na Dharau, na badala yake kudumisha Uhuru na Umoja, Haki na Usawa, Heshima na Utu;

**NA KWA KUWA** tunatambua kwamba mafundisho na mawazo ya Kimapinduzi yatalindwa, yataendelezwa na kudumishwa kwa misingi ya Kidemokrasia;

**NA KWA KUWA** tunatambua kuwa mapambano ya kujenga Ujamaa katika Zanzibar na kushiriki kwetu kikamilifu katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar kunahitaji SHERIA madhubuti itakayowaongoza watu Ki Katiba, kutokana na fikra za Wafanyakazi na Wakulima;

# SURA YA KWANZA
# ZANZIBAR

## Sehemu ya Kwanza
## Zanzibar

**1.** Zanzibar ni Nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vilivyoizunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Zanzibar na mipaka yake. *Kif. 3 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**2.** Zanzibar ni miongoni mwa Nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Zanzibar na Muungano. *Kif. 4 cha Sheria Nam.9/2010.*

**2A.** Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali, Rais aweza kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mikoa na Wilaya za Zanzibar. *Kif. 5 cha Sheria Nam.9/2010*

**3**.-(1) Kutakuwa na Muhuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao alama yake itakuwa kama itavyokubaliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Muhuri wa Serikali na alama nyenginezo.

(2) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na uwezo wa kuweka kitu chochote kitachokuwa kielelezo cha Serikali kama itavyokubaliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

**4.** Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote na isipokuwa kutokana na kifungu cha 80 ikiwa sheria yoyote inatofautiana na Katiba hii, basi Katiba hii ndiyo itayokuwa na nguvu na sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kinahitilafiana.

Katiba ya Zanzibar.

Zanzibar kufuata mfumo wa vyama vingi.
*Kif. 3 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**5.** Zanzibar itafuata mfumo wa Kidemokrasia wa Vyama Vingi vya Siasa wenye kuheshimu utawala wa sheria, haki za binaadamu, usawa, amani, haki na uadilifu.

Mgawanyo wa madaraka
*Kif. 4 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**5A** (1) Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu, Mamlaka ya Utendaji, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki.

(2) Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mamlaka ya kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki ni Mahkama.

(3) Hakuna mamlaka itakayoingilia Mamlaka nyengine isipokuwa kama na kwa kadri ilivyoelezwa katika Katiba hii.

## Sehemu ya Pili
## Watu

Mzanzibari.
*Kif. 5 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**6**.-(1) Kutakuwa na Mzanzibari ambaye upatikanaji wake, upoteaji wake na urudishwaji wake atakuwa kama alivyoainishwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Kila Mzanzibari, kwa misingi ya Katiba hii, ataweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki Mzanzibari, na atapaswa kutekeleza wajibu, majukumu na dhamana za Mzanzibari kama ilivyo kwenye Katiba hii au kwenye sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Haki ya kupiga Kura.
*Kif. 6 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**7.-**(1) Kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar na wananchi. Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki pamoja na masharti mengine ya Katiba hii na ya sheria inayotumika Zanzibar kuhusu mambo ya uchaguzi.

(2) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga sheria na kuweka masharti yanayoweza kuzuia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura kutokana na yoyote kati ya sababu zifuatazo, yaani Mzanzibari huyo:

(a) kuwa na uraia wa nchi nyengine;

(b) kuwa na ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Mahkama Kuu;

(c) kutiwa hatiani na kuendelea kutumikia adhabu kwa kosa la jinai katika Chuo cha Mafunzo, isipokuwa kwamba mtu aliyewekwa rumande atakuwa na haki ya kuandikishwa kupiga kura;

(d) kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura.

(3) Baraza la Wawakilishi litatunga sheria ya Uchaguzi inayohusu uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani wa Serikali za Mitaa na kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo:

(a) kuanzisha daftari la kudumu la wapiga kura na kuweka utaratibu wa kurekebisha yaliyomo katika daftari hilo;

(b) kutaja sehemu, nyakati za kuandikisha wapiga kura na muda wa ukaazi, katika Jimbo la Uchaguzi kwa ajili ya kupiga kura;

(c) utaratibu wa kumwezesha mpiga kura aliyejiandikisha sehemu moja kupiga kura sehemu nyengine na kutaja masharti ya utekelezaji wa utaratibu huo;

(d) kutaja kazi na shughuli za Tume ya Uchaguzi na utaratibu wa kila uchaguzi ambao utaendeshwa chini ya uongozi na usimamizi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(4) Mbali na sababu zilizoelezwa katika kifungu hiki hakuna sababu nyengine yoyote inayoweza kumzuia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura.

## SURA YA PILI

## Malengo na Maamuru Muhimu ya Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Wajibu mkubwa wa Serikali.

**8**. Itakuwa ni wajibu wa vyombo vyote vya Serikali pamoja na vyombo vyengine vyenye uwezo pamoja na watu wenye kutunga sheria kiutawala au uwezo wa kimahkama kufuata misingi ya uhuru, haki na amani.

Serikali na watu. *Kif. 6 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**9**.-(1) Zanzibar itakuwa ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii.

(2) Kwa hivyo hapa inaelezwa rasmi kwamba:

(a) mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuatana na Katiba utatoka kwa wananchi wenyewe;

(b) usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndiyo lengo kubwa la Serikali;

(c) Katiba hii itahakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika Serikali yao.

(3) Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Umoja wa Kitaifa na utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja nchini na lengo la kufikia demokrasia.

Malengo ya kisiasa. *Kif. 7 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**10**. Kwa madhumuni ya kuendeleza umoja na maendeleo ya watu na ustawi wa jamii katika nchi itakuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:-

(a) kutoa huduma za kutosha kwa ajili ya kuendeleza watu katika njia za mtu kuwa huru kwenda atakapo na utoaji huduma kwa watu wote na kutoa haki zote za kuishi kwa Mzanzibari sehemu zote za Zanzibar;

(b) kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa cheo dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka;

(c) kusimamia maendeleo ya uchumi wa nchi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyowekwa na Katiba, kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, kuratibu na kusimamia uendeshaji wa rasilimali muhimu za nchi;

(d) kutoa mwongozo na kuhakikisha maendeleo ya uchumi yenye urari na yaliyopangika na kwamba mfumo wa kiuchumi hautafanyika katika utaratibu utakaopelekea kulimbikiza kwa utajiri na njia za kuzalisha mali kwa watu wachache au kikundi fulani;

(e) kuhakikisha kwamba kila raia atakuwa na haki sawa, majukumu na fursa sawa kwa mujibu wa sheria, utu wa mtu utaheshimiwa na heshima ya mtu itaenziwa na kuendelezwa na kwamba uhuru, kutopendelea na uaminifu wa Mahkama pamoja na kupata fursa kwa urahisi ya kwenda katika Mahkama hizo kutapatikana na kuheshimiwa;

(f) kuhakikisha kwamba zipo huduma za kutosha za kiafya kwa watu wote, zipo fursa sawa na za kutosha za kielimu katika madaraja yote na kwamba utamaduni wa Zanzibar unalindwa, unaimarishwa na unaendelezwa;

(g) kwamba kila mtu mwenye uwezo wa kufanyakazi ana fursa ya kufanya kazi, na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali inayompatia mtu riziki yake, na kwamba msaada unatolewa kwa wale wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na walemavu;

(h) vyeo vyote vya madaraka ni dhamana na vipo kwa faida na manufaa ya umma na wale wote walio na madaraka watawajibika ama moja kwa moja kwa umma au kupitia kwa vyombo vya uwakilishi;

(i) vyombo vyote vya Serikali na watumishi wake vitaongozwa na vitazingatia Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Binaadamu na misingi ya utawala ulio bora.

Mabadiliko ya masharti ya Sura ya Pili.
*Kif. 8 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**10A**. Masharti ya Sehemu hii ya Sura hii hayatatiliwa nguvu ya kisheria na Mahkama yoyote, na Mahkama yoyote nchini haitakuwa na uwezo wa kuamua juu ya suala kama kutenda au kukosa kutenda jambo kama mtu au mamlaka yoyote au kama sheria au hukumu yoyote, inaambatana na masharti ya Sehemu hii ya Sura hii.

## SURA YA TATU

### Kinga ya Haki za Lazima, Wajibu na Uhuru wa Mtu Binafsi

**11**.-(1) Binaadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa. Usawa wa Binaadamu.

(2) Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

**12**.-(1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Usawa mbele ya Sheria. *Kif. 9 cha Sheria Nam. 2/2002 na Kif. 8 cha Sheria Nam.9/2010*

(2) Hakuna sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni cha ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taathira yake.

(3) Haki za raia, wajibu wa maslahi ya kila mtu yatalindwa na kuamuliwa na Mahkama pamoja na vyombo vya nchi na vyenginevyo vilivyowekwa na sheria.

(4) Hakuna mtu atakayebaguliwa na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi ya Afisi yoyote ya Serikali au uongozi mwengine wa chama chochote na vyombo vyake.

(5) Katika kifungu hiki neno "kubagua" maana yake ni kutimiza haja kwa watu mbali mbali kwa kutegemea utaifa wao, kabila, jinsia, ulemavu**,** pahala walipotokea, muelekeo wao kisiasa, rangi au dini ambapo watu wa aina fulani wanaonekana kuwa ni dhaifu na duni au wawekewe vikwazo na pingamizi ambavyo wale watu wa aina nyengine hawawekeani au wanapewa fursa au faida ambayo hawapewi watu wa aina nyengine.

Isipokuwa kwamba neno "kubagua" halitafafanuliwa kwa namna ambayo itazuia Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahsusi katika jamii.

(6) Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria Serikali itaweka taratibu zinazofaa na zitakazozingatia misingi kwamba:

(a) wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa Mahkama au chombo kinginecho kinachohusika basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa na pia haki ya kukata rufaa au ya kupata kitulizo kinginecho cha kisheria kutokana na maamuzi ya Mahkama au chombo hicho kinginecho kinachohusika;

(b) mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai hatatendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo;

(c) ni marufuku kwa mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho alipokitenda hakikuwa ni kosa chini ya sheria, na pia itakuwa ni marufuku kwa adhabu kutolewa ambayo ni kubwa kuliko adhabu iliyokuwepo wakati kosa linalohusika lilipotendwa;

(d) kwa ajili ya kuhifadhi haki ya usawa wa binadamu katika shughuli zote zinazohusu upelelezi na uendeshaji wa mambo ya jinai, katika shughuli nyenginezo ambapo mtu anakuwa chini ya ulinzi bila ya uhuru, na katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu, heshima ya utu wa mtu itatunzwa;

(e) kesi za jinai zinasikilizwa na hukumu kusomwa haraka; na

(f) mtuhumiwa katika kesi za jinai anapata fursa ya utetezi wa Wakili aliyemchagua yeye mwenyewe.

Haki ya kuwa hai. *Kif. 10 cha Sheria Nam. 2/2002*

**13**.-(1) Kila mtu anayo haki ya kuwa na hifadhi ya maisha yake.

(2) Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.

(3) Ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha.

Haki ya uhuru wa mtu binafsi.

**14**.-(1) Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru.

(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vyenginevyo isipokuwa tu:

(a) katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria; au

(b) katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na Mahkama kutokana na shauri au kosa la jinai ambalo mtu amekutwa na hatia ya kulitenda.

Haki ya faragha ya mtu na usalama wake.

**15**.-(1) Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake; maisha yake binafsi na ya nyumbani kwake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake.

(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa mujibu wa kifungu hiki, Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, namna ya kiasi ambacho haki ya mtu na faragha na usalama wa nafsi yake, mali yake na maskani yake, yaweza kuingiliwa bila ya kuathiri kifungu hiki cha Katiba hii.

Kinga ya uhuru wa kwenda.

**16.-**(1) Hakuna mtu atakayenyimwa uhuru wake wa kwenda, na kwa madhumuni ya kifungu hiki uhuru uliotajwa humu maana yake ni haki ya kwenda popote katika Zanzibar, haki ya kuishi katika sehemu yoyote ya Zanzibar, haki ya kuingia Zanzibar, haki ya kuondoka Zanzibar na kinga ya kutofukuzwa Zanzibar.

(2) Kizuizi cha kutokutembea kwa mtu yeyote kutokana na kuwekwa ndani kwake kisheria, haitochukuliwa kuwa inapingana au ni kinyume na kifungu hiki.

Kinga kutokana na kudhulumiwa mali.

**17**. Hakuna mali ya mtu yeyote itayochukuliwa kwa nguvu na hakuna maslahi au haki yoyote inayotokana na mali hiyo itayochukuliwa kwa nguvu isipokuwa pale ambapo masharti yafuatayo yametimizwa, yaani:

(a) kumilikiwa au kuchukuliwa kwa mali hiyo ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi, usalama wa wananchi, mazingira ya afya, kuimarisha maendeleo ya upangaji wa mji pamoja na kuendeleza mambo ambayo yataleta faida kwa wananchi kwa ujumla;

(b) umuhimu wa kuchukuliwa kitu hicho ni mkubwa sana hata kwamba unahalalisha uchukuaji wake hata kama utampa ugumu na matatizo mwenye mali hiyo; na

(c) sheria imewekwa kuhusiana na umilikaji au uchukuaji huo kwa kutoa fidia inayolingana.

**18**.-(1) Bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, na kutafuta kupokea na kutoa habari na dhana kupitia chombo chochote, bila ya kujali mipaka ya nchi, na pia ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati.

Uhuru wa maoni.

(2) Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii.

**19.-**(1) Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, wa imani na wa uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa kubadilisha dini au imani yake.

Uhuru wa mtu kuamini dini atakayo. *Kif. 11 cha Sheria Nam. 2/2002.*

(2) Bila ya kuathiri sheria zinazohusika kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa huru na jambo la hiari ya mtu binafsi; na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za Mamlaka ya nchi.

(3) Kila palipotajwa neno "dini" katika kifungu hiki ifahamike kwamba maana yake ni pamoja na madhehebu ya dini, na maneno mengineyo yanayofanana au kuambatana na neno hilo nayo yatatafsiriwa kwa maana hiyo.

**20**.-(1) Isipokuwa kwa hiari yake, hakuna mtu atakayezuiwa kufurahia uhuru wake wa kuchanganyika au kujiunga yaani haki yake ya kuchanganyika na kujihusisha atakavyo na watu wengine na hasa kuunda au kuwa mwanachama wa vyama vya wafanyakazi, vyama vya haki za binadamu au vyama vyengine kwa faida yake na ambavyo vimekubaliwa kisheria.

Kinga kwa uhuru wa kujikusanya na kujiunga. *Kif. 12 cha Sheria Nam. 2/2002.*

(2) Hakuna chochote kilichomo ndani ya au kufanywa chini ya sheria yoyote kitakachohesabiwa kuwa hakilingani au ni kinyume na kifungu hiki (katika kiwango ambacho sheria mama inaeleza):

(a) mambo yanayotakiwa kwa faida ya ulinzi, usalama wa raia, mazingira ya afya na jamii;

(b) mambo yanayotakiwa kwa madhumuni ya kulinda haki na uhuru wa watu wengine;

(c) mambo yanayotakiwa kuweka makatazo fulani kwa maafisa wa Serikali, Wanajeshi au watu wanaofanya kazi waliochaguliwa kwa hiari.

Uhuru wa kushiriki shughuli za umma, haki ya kufanya kazi na kupata ujira.

**21**.-(1) Kila Mzanzibari anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia Wawakilishi waliochaguliwa kwa hiari.

(2) Kila Mzanzibari anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye maisha yake au yanayolihusu Taifa.

(3) Kila Mzanzibari anayo haki ya kufanya kazi na anastahili fursa na haki sawa, kwa masharti ya usawa ya kushika nafasi yoyote ya kazi na shughuli yoyote iliyoko chini ya Mamlaka ya Zanzibar.

(4) Kila mtu, bila ya kuwapo ubaguzi wa aina yoyote, anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake na watu wote wafanyao kazi kulingana na uwezo wao watapata malipo kulingana na kiasi ya sifa za kazi wanayoifanya.

Wajibu wa kushiriki kazini. Kif.13 cha Sheria Nam. 2/2002.

**22**.-(1) Kazi pekee ndiyo huzaa utajiri wa mali katika jamii, ndio chimbuko la ustawi wa wananchi na kipimo cha utu, kila mtu anao wajibu wa:

(a) kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi halali na ya uzalishaji mali; na

(b) kutimiza nidhamu ya kazi na kujitahidi kufikia malengo ya uzalishaji ya binafsi na ya pamoja yanayotakiwa au yaliyowekwa na sheria.

(2) Bila ya kujali masharti ya kijifungu cha (1) hakutakuwepo na kazi ya shurti katika Zanzibar.

Wajibu wa kutii sheria za nchi, kulinda mali ya umma na ulinzi wa Taifa.

**23**.-(1) Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na sheria za Zanzibar, kuchukua hatua za kisheria kama zilivyowekwa, kuhakikisha hifadhi ya Katiba na Sheria za nchi.

(2) Kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Zanzibar, mali ya nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwengine.

(3) Watu wote watatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kwa pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadae ya Taifa lao.

(4) Kila Mzanzibari anawajibu wa kulinda, kuhifadhi kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa Zanzibar.

(5) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga sheria zinazofaa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kutumikia katika majeshi na katika ulinzi wa Taifa.

Mipaka kwa haki na uhuru, na hifadhi kwa haki na wajibu wake. Kif. 14 cha Sheria Nam 2/2002 na Kif. 9 cha Sheria Nam. 9/2010.

**24**.-(1) Haki na Uhuru wa binadamu ambayo misingi yake imeorodheshwa na Katiba hii haitatumiwa na mtu mmoja kwa namna ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma na inaweza kubanwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi iwapo tu kibano hicho ni lazima na kinakubalika katika mfumo wa kidemokrasia. Kwa vyovyote vile kibano hicho:

(a) hakitaingilia haki ya kutokuteswa, kutoadhibiwa kinyama na kutokudhalilishwa; au

(b) hakitaingilia misingi ya haki yenyewe; au

(c) hakitaiIetea jamii athari zaidi ya iliyopo kutokana na jambo ambalo kibano hicho kinalenga.

(2) Mtu yeyote anayedai kuwa sharti lolote katika Sehemu hii ya Sura hii au katika sheria yoyote inayohusu haki yake au wajibu wake limevunjwa, linavunjwa au inaelekea litavunjwa na mtu yeyote Zanzibar, anaweza kufungua shauri katika Mahkama Kuu. Mahkama Kuu itakuwa na uwezo wa kutoa tamko na kuamuru nafuu au fidia kwa mtu yeyote anayehusika.

(3) Rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahkama Kuu katika shauri lililofunguliwa dhidi ya masharti ya Sura hii ya Katiba yatasikilizwa na Mahkama Kuu mbele ya Majaji watatu bila ya kumjumuisha Jaji aliyeamua shauri hilo mara ya kwanza. Majaji hao watatu watateuliwa na Jaji Mkuu na uamuzi wao utakuwa ni wa mwisho na hautokatiwa rufaa kwenye Mahkama ya Rufaa ya Tanzania.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii, Mahkama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusikiliza kwa mara ya kwanza shauri lolote lililoletwa mbele yake kwa kufuata kifungu hiki, na Mamlaka ya nchi yaweza kuweka sheria kwa ajili ya:

(a) kusimamia utaratibu wa kufungua mashauri kwa mujibu wa kifungu hiki;

(b) kufafanua uwezo wa Mahkama Kuu katika kusikiliza mashauri yaliyofunguliwa chini ya kifungu hiki;

(c) kuhakikisha utekelezaji bora wa madaraka ya Mahkama Kuu, hifadhi na kutilia nguvu, haki, uhuru na wajibu kwa mujibu wa Katiba hii.

Haki za lazima na uhuru wa binafsi.

**25**.-(1) Ilivyokuwa kila mtu wa Zanzibar anawajibika kupata haki zake za lazima na uhuru wa binafsi bila ya kujali kabila, pahali alipotoka au maskani au mahusiano mengine yoyote yale, mtazamo wa kisiasa alionao, rangi, dini au jinsi, lakini mradi iwe uhuru wake unaheshimu haki na uhuru wa wengine na iwe kwa faida ya jamii, basi atakuwa na haki kupata kwa kila kimoja kwa vyote vya hivi vifuatavyo:

(a) maisha yake, uhuru wake, usalama wake na kulindwa na sheria;

(b) uhuru wa kufikiri, wa kujieleza, wa mkusanyiko na mchanganyiko; na

(c) haki ya kuweza kukaa faragha katika nyumba yake na kulindwa kwa mali yake pamoja na kutokuchukuliwa mali hiyo bila kupewa fidia ipasavyo.

(2) Maelezo ya Sura hii yatakuwa na madhumuni ya kuwezesha kulinda haki hizo na uhuru kulingana na mipaka maalumu ya haki hizo na uhuru kama ilivyoelezwa katika vifungu vinavyohusika kwa mipaka iliyowekwa ili kuhakikisha kwamba kutumika kwa haki hizo na uhuru huo wa mtu binafsi hakuathiri haki na uhuru wa wengine au maslahi ya Taifa kwa ujumla.

Kufungua mashauri.
*Kif. 15 cha Sheria Nam. 2/2002 na Kif. 10 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**25A.**-(1) Mtu yeyote anaweza kufungua shauri katika Mahkama Kuu iwapo ataona kuwa Katiba hii imevunjwa au inavunjwa au inaelekea kuvunjwa. Mahkama Kuu itakuwa na uwezo wa:-

(a) kumtaka Afisa yeyote au chombo chochote cha Serikali kutoa taarifa inayohitajika na Mahkama Kuu yaweza kufanya hivyo kwa kuombwa au kwa uamuzi wake yenyewe;

(b) kutamka na kutoa amri kuwa Katiba hii imevunjwa, inavunjwa au inaelekea kuvunjwa, na Mahkama Kuu inaweza kutoa maagizo kwa Afisa anayehusika au chombo cha Serikali kinachohusika.

(2) Rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahkama Kuu katika shauri lililofunguliwa dhidi ya masharti ya kifungu hiki itasikilizwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 24(3) cha Katiba.

## SURA YA NNE

## Serikali

### Sehemu ya Kwanza

### Rais

Afisi ya Rais na sifa za kuchaguliwa kuwa Rais.
*Kif. 3 cha Sheria Nam. 13/1992 na Kif. 11 cha Sheria Nam. 9/2010..*

**26.**(1) Kutakuwa na Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mkuu wa Nchi ya Zanzibar, Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(2) Mtu yeyote anaweza kufaa kuchaguliwa kuwa Rais ikiwa:

(a) ni Mzanzibari wa kuzaliwa; na

(b) ameshatimia umri wa miaka 40; na

(c) anazo sifa za kumuwezesha kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(d) ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa kilichosajiliwa rasmi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya 1992.

Uchaguzi wa Rais.
*Kif. 12 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**27**.-(1) Rais atachaguliwa kufuatana na Katiba hii na kwa mujibu wa sheria yoyote itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi kuhusu uchaguzi wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(2) Uchaguzi wa Rais utafanyika katika tarehe itayowekwa na Tume ya Uchaguzi.

(3) Kwa madhumuni ya uchaguzi huo, Zanzibar itahesabika kuwa ni jimbo moja. Mtu yeyote aliyejiandikisha kupiga kura katika kumchagua Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi atakuwa na uwezo wa kupiga kura katika uchaguzi wa Rais.

Muda wa kuendelea na Urais.
*Kif. 13 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**28**.(1) Kufuatana na Katiba hii mtu ataendelea kuwa Rais mpaka:

(a) Rais anayefuata ale kiapo cha kuwa Rais; au

(b) afariki wakati akiwa Rais; au

(c) hapo atapojiuzulu; au

(d) iwapo amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; au

(e) kwa sababu yoyote nyengine ameacha kuwa Kiongozi kwa mujibu wa vifungu vyengine vya Katiba hii.

(2) Kufuatana na maelezo ya kijifungu (1) cha kifungu hiki, Rais ataacha madaraka yake baada ya kumalizika miaka mitano kuanzia tarehe, ambapo:

(a) kama yeye ni mtu ambaye ndiye mara ya kwanza amechaguliwa kuwa Rais chini ya Katiba hii alipokula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kuwa Rais; na

(b) kwa sababu nyenginezo mtu wa mwisho kushika madaraka hayo kwa mujibu wa Katiba hii alipokula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kuwa Rais, au pasingelikuwa na sababu ya kifo chake, basi angalikula kiapo hicho.

(3) Bila ya kuathiri chochote kilichomo katika kifungu hiki cha Katiba hii hakutakua na mtu yeyote ataechaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar kwa zaidi ya vipindi viwili vya miaka mitano kila kimoja.

Kuongezwa kwa kipindi cha miaka mitano. *Kif. 14 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**29.** Ikiwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imo katika vita na ikiwa Rais anaona kuwa ni muhimu kuzuia uchaguzi, Baraza la Wawakilishi linaweza kwa kupitisha azimio, kuzidisha muda wa miaka mitano uliotajwa kwenye kijifungu (2) cha kifungu cha 28 katika kipindi hadi kipindi lakini hakutakuwa na kipindi kitakachozidi miezi sita mfululizo.

Kutofaa kuwa Rais. *Kif. 15 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**30**.-(1) Mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Rais ikiwa:

(a) amefanya kitendo chochote, au hitilafu yoyote ambapo kama angekuwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kungemfanya asite kuwa Mjumbe wa Baraza hilo;

(b) amechaguliwa kushika madaraka hayo katika vipindi viwili vilivyokwisha,

Isipokuwa kwamba kijifungu hiki kisitafsirike kuwa kinamzuia mtu huyo kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Katika muda wake wa Urais, Rais hatashika madaraka yoyote mengine yenye mapato isipokuwa yale ya Urais.

Kiapo cha Rais.

**31**.-(1) Mtu anayechukua madaraka ya Urais, kabla ya kuanza wadhifa huo, atakula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kazi kama kitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi lakini kwa hali yoyote itabidi ashike madaraka hayo kabla ya kupita siku saba baada ya kuchaguliwa.

(2) Viapo hivyo vilivyotajwa vitaendeshwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar au iwapo hayupo, vitaendeshwa na mtu anayeshikilia nafasi hiyo.

Kuachishwa Urais kwa ugonjwa.

*Kif. 16 Sheria Nam. 9/2010.*

**32.-**(1) Suala lolote la kwamba Rais au mtu yeyote anayefanya kazi au kutaka kufanya kazi za Rais, hawezi kwa sababu ya maradhi ya kimwili au kiakili, itaamuliwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

(2) Iwapo suala ni kwamba Rais hawezi kufanya kazi zake kwa maradhi ya kimwili au kiakili na ikiwa Jaji Mkuu ameombwa na Baraza la Mapinduzi, kushughulikia suala hilo, hapo:-

(a) Jaji Mkuu atateua Kamati ambayo itakuwa na watu si chini ya watano ambao kati yao ni Madaktari na watu wawili wanaofaa kuwa Majaji wa Mahkama Kuu;

(b) Kamati hiyo itafanya utafiti kuhusiana na hali ya Rais na baadaye itapeleka ripoti yake kwa Jaji Mkuu ikieleza maoni yake iwapo Rais huyo kwa maradhi aliyonayo ya kimwili au akili, kama hawezi kufanya kazi za Urais; na

(c) Jaji Mkuu atathibitisha kwa kadri aonavyo baada ya kuitafakari ripoti ya Kamati na atapeleka hati

ya uthibitisho kwamba Rais hawezi kumudu kufanya kazi zake kutokana na maradhi ya kimwili au akili kwa Baraza la Mapinduzi na kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi na iwapo Jaji Mkuu hatabatilisha uthibitisho wake ndani ya siku saba kutokana na Rais kupata nafuu na kurejea kazini, basi itahesabiwa kwamba kiti cha Rais kiwazi kwa mujibu wa kifungu cha 33(1)(c) cha Katiba na masharti yaliyomo katika kifungu cha 34(1) cha Katiba yatatumika.

Nafasi katika kiti cha Urais. *Kif. 17 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**33**.(1) Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kwa:

(a) kufariki; au

(b) kujiuzulu; au

(c) maradhi ya kimwili au kiakili; au

(d) sababu nyengine yoyote itakayomfanya Rais kushindwa kutekeleza kazi za Rais,

watu wafuatao, kwa mujibu wa mpangilio, watashika nafasi hiyo:

(i) Makamo wa Pili wa Rais, au ikiwa hayupo;

(ii) Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye anatoka katika chama anachotoka Rais na yeye ikiwa hayupo;

(iii) Jaji Mkuu wa Zanzibar.

(2) Iwapo kiti cha Urais:

(a) kwa sababu Rais anataka kuondoka Tanzania; au

(b) kwa sababu nyengine yoyote ile,

Rais anaweza kwa maandishi na kufuatana na masharti atakayoainisha atayatoa madaraka yake kwa mujibu wa mpangilio, kwa:

(i) Makamo wa Pili wa Rais au naye ikiwa hayupo;

(ii) Mjumbe mmoja wa Baraza la Mapinduzi ambaye Rais ataona anafaa.

(3) Iwapo mtu yeyote anafanya shughuli za Rais chini ya vijifungu (1) na (2) vya kifungu hiki, ataendelea kufanya shughuli hizo mpaka ataporejea mmoja ya watu waliomtangulia katika kijifungu cha (1) cha kifungu hiki mpaka hapo atapochaguliwa Rais mwengine au kwa shughuli za kijifungu cha (2) hadi hapo Rais ataporejea nchini au atapobatilisha uwezo huo alionao.

Mpango wa uchaguzi iwapo kiti cha Rais kiwazi. *Kif.4 Sheria Nam. 13/1992, Kif.2 cha Sheria Nam. 11/1995, na Kif. 18 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**34**.-(1) Endapo kiti cha Rais kiwazi kwa sababu ya kufariki au kujiuzulu au kwa maradhi chini ya kifungu cha 33 cha Katiba hii, nafasi hiyo itajazwa kama ifuatavyo:

(i) iwapo Rais aliyekuwapo ametumikia kwa muda wa chini ya miaka minne basi mtu anayemfuatia kwa madaraka kwa mujibu wa kifungu cha 33(1) cha Katiba atachukua madaraka ya Urais kwa muda na uchaguzi utaitishwa ndani ya siku mia moja na ishirini, na uchaguzi huo utaendeshwa kwa utaratibu ulioelezwa katika vijifungu vya (2) hadi (7) vya kifungu hiki;

(ii) iwapo Rais aliyekuwepo ametumikia Urais kwa miaka minne au zaidi, basi mtu anayemfuatia kwa madaraka atachukua madaraka ya Urais na ataendelea na madaraka hayo kwa kipindi kilichobaki cha muda wa Urais.

(iii) mtu atayechukua madaraka hayo ya Urais atakuwa na madaraka yote ya Rais, kwa mujibu wa Katiba na atateua Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, Mawaziri na Viongozi wengine kadri atavyoona inafaa.

(iv) bila ya kujali masharti ya vifungu vya 28(3) na 30(1)(b) vya Katiba, endapo mtu anayemfuata Rais kwa madaraka atashika kiti cha Rais kwa kipindi kinachopungua miaka minne ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara mbili, lakini kama atashika kiti cha Rais kwa muda wa miaka minne au zaidi ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara moja tu.

(2) Litokeapo jambo lolote lilotajwa katika Katiba na kulazimu uchaguzi wa Rais kufanyika, kila chama cha siasa kinachopenda kushiriki katika uchaguzi wa Rais kitawasilisha kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kwa mujibu wa Sheria, jina la mwanachama wake mmoja kinayetaka asimame kama mgombea katika uchaguzi wa Rais wa Zanzibar.

(3) Mapendekezo ya majina ya wagombea katika uchaguzi wa Rais yatawasilishwa kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar katika siku na saa itakayotajwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na mtu hatakuwa amependekezwa kwa halali isipokuwa tu kama kupendekezwa kwake kumeungwa mkono na wananchi wapiga kura kwa idadi na kwa namna itakayotajwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(4) Endapo inapofika siku na saa iliyotajwa kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya majina ya wagombea, ni mgombea mmoja tu ambaye amependekezwa kwa halali, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, itawasilisha jina lake kwa wananchi, nao watapiga kura ya kumkubali au kumkataa, kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki na ya Katiba.

(5) Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar utafanywa siku itakayoteuliwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(6) Mambo mengine yote yahusuyo utaratibu wa uchaguzi wa Rais yatakuwa kama itakavyofafanuliwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo.

(7) Iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwamba amechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa kifungu hiki, basi hakuna Mahkama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake.

Mshahara na malipo mengine ya Rais.

**35.-**(1) Rais atapokea mshahara na posho, na anapostaafu atapata malipo ya uzeeni, kiinua mgongo au posho, kama itakavyoamuliwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Mshahara na posho la Rais hautopunguzwa wakati akiwa bado ni Rais.

(3) Pesa zote zilizoainishwa na kifungu hiki zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

Rais hatashtakiwa akiwa kazini.

**36.**(1) Hakuna mashtaka yoyote ya jinai yatakayofunguliwa au kuendelezwa dhidi ya Rais wakati akiwa kazini, au dhidi ya mtu yeyote ambaye anafanya kazi ya Urais, kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Katiba hii.

(2) Hakuna mashtaka ya kihukukia ambapo kuna madai kuhusiana na kitu chochote kilichotendwa au kuachwa kutendwa yatakayoanzishwa na kuendelezwa dhidi ya Rais wakati akiwa kazini, au dhidi ya yeyote anayefanya kazi za Urais.

(3) Iwapo kuna sheria imewekwa ambayo inaweka muda maalum ambapo mashtaka ya aina yoyote yanaweza kuanzishwa dhidi ya mtu yeyote muda wote ambapo mtu anakuwa Rais au kufanyakazi za Rais hautahesabiwa kuwa ni muda maalum kuhusiana na sheria hiyo iwapo mashtaka yoyote ya aina kama yaliyotajwa katika kijifungu cha (1) au (2) ni dhidi ya mtu huyo.

Baraza la Wawakilishi laweza kumshtaki Rais.
*Kif. 5 cha Sheria Nam 13/1992 na Kif. 19 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**37**.-(1) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 36 cha Katiba hii, Baraza la Wawakilishi linaweza kupitisha azimio la kumuondoa Rais madarakani endapo itatolewa hoja ya kumshtaki Rais na ikapitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya kifungu hiki, hoja yoyote ya kumshtaki Rais haitotolewa isipokuwa tu kama inadaiwa kwamba Rais ametenda vitendo vinavyovunja Katiba au amekuwa na mwenendo unaodhalilisha kiti cha Rais, na haitatolewa hoja ya namna hiyo ndani ya miezi kumi na mbili tangu hoja kama hiyo ilipotolewa na ikakataliwa na Baraza la Wawakilishi.

(3) Baraza la Wawakilishi halitapitisha hoja ya kumshtaki Rais isipokuwa tu kama:

(a) taarifa ya maandishi iliyotiwa sahihi na kuungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasiopungua nusu ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi itatolewa kwa Spika siku thalathini kabla ya kuwasilishwa katika Baraza

la Wawakilishi ikifafanua makosa aliyoyatenda Rais, na ikipendekeza kuwa Kamati Maalum ya Uchunguzi iundwe ili isikilize shauri la kushtakiwa kwa Rais;

(b) wakati wowote baada ya Spika kupokea taarifa iliyotiwa sahihi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi itatolewa kwa Spika na kujiridhisha kwa masharti ya kuleta hoja yametimizwa, Spika atalitaka Baraza la Wawakilishi, bila ya majadiliano, lipige kura juu ya hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi na kama ikiungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasiopungua theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, atatangaza majina ya wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi;

(c) Kamati Maalum ya Uchunguzi, kwa madhumuni ya kifungu hiki, itakuwa na wajumbe wafuatao, yaani:

(i) Jaji Mkuu wa Zanzibar, ambaye ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;

(ii) Jaji wa Mahkama ya Rufaa ya Tanzania;

(iii) Jaji kutoka nchi yoyote ya Jumuiya ya Madola;

(iv) Wajumbe wanne wa Kamati ya Katiba na Sheria ya Baraza la Wawakilishi akiwemo Mwenyekiti.

(d) ndani ya siku saba baada ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuundwa, itakaa, ichunguze na

kuchambua mashtaka dhidi ya Rais na kisha mapema iwezekanavyo itatoa taarifa kwa Baraza la Wawakilishi kama kwa maoni yake mashtaka dhidi ya Rais yana msingi au hayana;

(e) Rais atakuwa na haki ya kujitetea na kuwakilishwa mbele ya Kamati Maalum ya Uchunguzi.

(4) Endapo Kamati Maalum ya Uchunguzi itatoa taarifa kwa Baraza la Wawakilishi kwamba jambo lolote katika mashtaka dhidi ya Rais halina msingi, basi Baraza la Wawakilishi halitaendelea kuishughulikia zaidi hoja ya kumshitaki Rais kuhusiana na jambo hilo.

(5) Endapo Kamati Maalum ya Uchunguzi itatoa taarifa kwa Baraza la Wawakilishi kwamba mashtaka dhidi ya Rais yana msingi, suala la kushtakiwa Rais litawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi zima, na Baraza la Wawakilishi laweza, baada ya mjadala, kwa kura za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasiopungua theluthi mbili za Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kupitisha azimio kuwa mashtaka dhidi ya Rais yamethibitika na kwamba hastahili kuendelea kushika kiti cha Rais, na hapo Rais atawajibika kujiuzulu kabla ya kwisha kwa siku tatu tangu Baraza la Wawakilishi lilipopitisha azimio hilo.

(6) Spika wa Baraza la Wawakilishi atawasilisha rasmi azimio hilo kwa Rais pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(7) Hakuna shughuli zozote kwa mujibu wa kifungu hiki zitakazoanzishwa au zitakazoendelezwa wakati wowote ambapo Baraza la Wawakilishi litakua limeahirishwa.

(8) Endapo Rais ataacha kushika kiti cha Rais kutokana na mashtaka dhidi yake kuthibitika, basi:-

(i) hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya pencheni wala kupata haki au nafuu nyenginezo alizonazo kwa mujibu wa Katiba au sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi; na

(ii) hataweza kugombea tena nafasi ya Urais au Uwakilishi kwa muda wa miaka mitano tokea siku aliyoachishwa Urais.

Isipokuwa pindi Rais huyo akiwa ameshatumikia kipindi cha miaka mitano ya awali na akakutwa na mashtaka katika kipindi cha pili basi atapata nusu ya haki na nafuu nyengine alizonazo kwa mujibu wa Katiba au sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Hadhi ya Rais aliyepita.

**38**. Itakuwa ni jukumu la Serikali kulinda hadhi ya mtu yeyote atakaeacha kiti cha Urais kwa sababu ya kutochaguliwa tena, muda wake kumalizika, kujiuzulu au kwa sababu nyengine yoyote iliyochini ya misingi ya Katiba hii kama itavyokubaliwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

## Sehemu ya Pili

## Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais

Makamo wawili wa Rais.
*Kif. 21 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**39**.-(1) Kutakuwa na Makamo Wawili wa Rais ambao watajulikana kama Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais.

(2) Ndani ya siku saba mara baada ya kushika madaraka, Rais atateua Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais.

(3) Makamo wa Kwanza wa Rais atatakiwa awe na sifa za kumuwezesha kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la

Wawakilishi na atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na chama kilichotokea nafasi ya pili katika matokeo ya kura ya Uchaguzi wa Rais.

Isipokuwa kwamba:-

(i) iwapo chama kilichotokea nafasi ya pili katika matokeo ya kura ya Uchaguzi wa Rais kimepata chini ya asilimia kumi (10%) ya kura zote za Uchaguzi wa Rais, au

(ii) endapo Rais atakuwa hana mpinzani,

basi nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itapewa chama chochote cha upinzani kilichotokea cha pili kwa wingi wa viti vya Majimbo katika Baraza la Wawakilishi.

(4) Makamo wa Kwanza wa Rais hatokuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(5) Makamo wa Kwanza wa Rais atakuwa ni Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na atafanya kazi zote atakazopangiwa na Rais.

(6) Makamo wa Pili wa Rais atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka katika chama anachotoka Rais.

(7) Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ndiye Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na pia atakuwa ndiye Kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

(8) Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais hawatoanza kazi mpaka waapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo chengine mbele ya Rais kama kitakavyoelezwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(9) Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais wakati wote watakapokuwa madarakani watawajibika kwa Rais.

Kuachwa wazi kwa nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. *Kif. 22 Sheria Nam. 9/2010.*

**39A**.-(1) Endapo, ndani ya siku saba mara baada ya Rais kushika madaraka, chama kinachostahiki kutoa Makamo wa Kwanza wa Rais, kitashindwa kuwasilisha kwa Rais jina la uteuzi wa Makamo wa Kwanza wa Rais, Rais, bila ya kujali masharti ya kifungu cha 39(1) na (3) cha Katiba, atawacha wazi nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na kuteua Makamo wa Pili wa Rais.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, Rais, bila ya kujali masharti ya kifungu cha 42 (2) cha Katiba, atateua Mawaziri na kuwacha wazi nafasi za uteuzi wa chama au vyama vya upinzani.

Kuwa wazi kwa nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais. *Kif. 23 Sheria Nam. 9/2010.*

**40**.(1) Endapo nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais itakuwa wazi:

(a) kwa sababu ya kufariki au kujiuzulu; au

(b) ikiwa Rais amefuta uteuzi huo; au

(c) kwa sababu nyengine yoyote itakayomfanya ashindwe kuwa na sifa za Makamo wa Kwanza au Makamo wa Pili wa Rais,

Rais atamteua Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais kutegemeana na nafasi iliyo wazi.

(2) Iwapo mtu atafutwa katika nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mujibu wa kijifungu cha (1)(b) cha kifungu hiki, chama chake si zaidi ya siku kumi na nne kitapendekeza kwa Rais jina la mtu mwengine.

Hoja ya kura ya kutokuwa na imani.
*Kif. 6 cha Sheria Nam 13/1992, Kif. 4 cha Sheria Nam 11/1995 na Kif. 24 Sheria Nam. 9/2010.*

**41**.-(1) Bila ya kujali masharti ya Katiba hii, Baraza la Wawakilishi linaweza kupitisha azimio la kura ya kutokuwa na imani na Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais endapo itatolewa hoja kupendekeza na ikapitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya kifungu hiki, hoja yoyote ya kutaka kupitisha kura ya kutokuwa na imani na Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais haitatolewa katika Baraza la Wawakilishi endapo:

(a) haijapita miezi sita tangu Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais kuteuliwa na Rais;

(b) haijapita miezi tisa tangu hoja ya namna hiyo ilipotolewa katika Baraza laWawakilishi na Baraza la Wawakilishi likakataa kuipitisha.

(3) Hoja ya kura ya kutokuwa na imani na Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais haitapitishwa na Baraza la Wawakilishi isipokuwa tu kama:

(a) taarifa ya maandishi, iliyotiwa sahihi na kuungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasiopungua nusu ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi itatolewa kwa Spika siku angalau kumi na nne kabla ya siku inapokusudiwa kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi;

(b) baada ya Spika kuridhika kwamba taarifa hiyo ya hoja inatimiza masharti yote ya Katiba hii na imefafanua sababu za kutokuwa na imani, basi itawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

(4) Endapo Spika ataridhika na akaamua kuwa hoja iwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi, basi hoja itawasilishwa na kuamuliwa na Baraza la Wawakilishi zima mapema iwezekanavyo na kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

(5) Azimio la hoja ya kura ya kutokuwa na imani na Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais litapitishwa na Baraza la Wawakilishi endapo hoja inaungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasiopungua theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi.

(6) Mapema iwezekanavyo, na kwa vyovyote vile ndani ya siku mbili tangu Baraza la Wawakilishi lilipopitisha Azimio la hoja ya kura ya kutokuwa na imani na Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais, Spika atawasilisha Azimio hilo kwa Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais atatakiwa kujiuzulu na Rais atamteua mjumbe mwengine wa Baraza la Wawakilishi kuwa Makamo wa Pili wa Rais.

(7) Endapo Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais ataacha kushika wadhifa wake huo kutokana na Azimio la hoja ya kura ya kutokuwa na imani:

(i) hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya pencheni wala kupata haki au nafuu nyenginezo, kwa mujibu wa Katiba au Sheria yoyote iliyotungwa na Baraza; na

(ii) atabaki kuwa Mwakilishi lakini hataweza kuteuliwa tena kuwa Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri au Mkuu wa Mkoa kwa kipindi chote cha uhai wa Baraza hilo.

## Sehemu ya Tatu

## Mawaziri, Naibu Mawaziri na Baraza la Mapinduzi

Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
*Kif. 25 cha Sheria Nam.*

**42**.-(1) Kutakuwa na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama zitakavyoanzishwa na Rais.

(2) Rais ndani ya kipindi cha siku kumi na nne mara baada ya kuteua Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, kwa kushauriana na Makamo wote Wawili wa Rais atateua Mawaziri kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia uwiano wa viti vya majimbo kwa vyama vya siasa vilivyomo ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Kuacha kufanya-kazi kwa Makamo wa Kwanza na Mawa-ziri.
*Kif.26 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**42A**. Endapo Makamo wa Kwanza wa Rais na, au Mawaziri kutoka vyama vya upinzani watajiuzulu au wataacha kutekeleza kazi zao kwa zaidi ya siku saba, Rais bila ya kujali masharti ya vifungu vya 39(3) na 42(2) vya Katiba, ataacha wazi nafasi za uteuzi wao, na iwapo nafasi hizo zitakuwa wazi kwa zaidi ya siku tisini, Rais anaweza kuteuwa Mawaziri wengine kujaza nafasi zao.

Baraza la Mapinduzi.
*Kif. 5 cha Sheria Nam 11/1995 Kif. cha 27 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**43**.-(1) Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi ambalo litajumuisha Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, Mawaziri pamoja na Wajumbe wengine kama Rais atakavyoona inafaa.

(2) Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(3) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atahudhuria mikutano yote ya Baraza la Mapinduzi na atakuwa na haki zote za Mjumbe wa Baraza hilo.

(4) Kazi za Baraza la Mapinduzi zitakuwa:

(a) kumsaidia na kumshauri Rais katika masuala ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(b) kuratibu shughuli za Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yao.

(5) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla, na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(6) Maelezo ya kijifungu cha (4) na (5) hayatatumika kuhusiana na:

(a) kuteuliwa na kuachishwa kazi kwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, Mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi na Naibu Mawaziri chini ya vifungu vya 39, 42 na 47 au kupewa dhamana kwa Waziri yoyote chini ya kifungu cha 44;

(b) kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi;

(c) kuhusiana na mambo yaliyotajwa katika kifungu cha 59 (yanayohusiana na uwezo wa kutoa msamaha).

Ugawaji wa Wizara kwa Mawaziri
*Kif. 28 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**44**.-(1) Majukumu kwa shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na utawala wa Idara yoyote ya Serikali yanaweza kuwekwa kwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais na Mawaziri wengine kama Rais atavyoidhinisha kwa maandishi.

(2) Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi ambao hawana Mawizara watakuwa Mawaziri wasio na Wizara Maalum.

Mikutano ya Baraza.
*Kif.29 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**45**.-(1) Rais akiwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ataongoza mikutano yote na ikiwa hayupo, Makamo wa Pili wa Rais atakuwa Mwenyekiti wa muda.

(2) Iwapo Makamo wa Pili wa Rais naye hayupo Zanzibar basi mikutano itasimamiwa na mtu anayeshikilia madaraka ya Urais.

(3) Kiwango cha kufanyika mkutano wa Baraza la Mapinduzi itakuwa ni theluthi mbili ya Wajumbe wote.

Viapo vya uaminifu.
*Kif.30 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**46**. Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi hataanza kufanyakazi zake, mpaka aapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo cha utekelezaji wa kazi zake mbele ya Rais kama vitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

Naibu Mawaziri.
*Kif.cha 31 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**47**. Rais anaweza kwa kushauriana na Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kuteua Naibu Mawaziri kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kumsaidia Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais na Mawaziri katika utekelezaji wa kazi zao na hawatoanza kazi zao mpaka kwanza waapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo cha utekelezaji wa kazi zao mbele ya Rais kama vitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

**48**. Nafasi ya Waziri, Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Naibu Waziri itakuwa wazi:

Nafasi ya Waziri, Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi kuwa wazi. *Kif.cha 32 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(a) endapo Rais atamwondosha kwenye madaraka hayo kwa hati yenye muhuri wa Rais; au

(b) iwapo mjumbe ameacha kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu nyengine zaidi ya kuvunjika kwa Baraza hilo; au

(c) endapo Rais atakubali ombi la kujiuzulu kwa mshika wadhifa huo; au

(d) mara baada ya Rais kushika madaraka.

**49**.-(1) Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi ambaye atakuwa pia Katibu Mkuu Kiongozi ataeteuliwa na Rais na ambaye ndiye atakayekuwa dhamana wa Afisi ya Baraza hilo na dhamana kwa mujibu wa maelekezo atakayopewa na Rais, kwa kupanga shughuli za mikutano pamoja na kuweka kumbukumbu ya mikutano hiyo, na kupeleka maamuzi yanayohusika kwa watu au vyombo vinavyohusika na atafanya kazi nyengine atakazopewa na Rais mara kwa mara.

Katibu wa Baraza la Mapinduzi. *Kif.33 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(2) Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa ndiye Kiongozi wa Utumishi wa Umma kwa Zanzibar na hatoanza kazi zake mpaka atakapoapishwa na Rais.

**50.-**(1) Pale Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais au Waziri yeyote mwengine anapokuwa na dhamana ya Wizara yeyote ya Serikali, atakuwa ndiye kiongozi na Msimamizi Mkuu na bila ya kuathiri masharti yoyote ya usimamizi, Katibu Mkuu ambaye afisi yake itakuwa ni ya utumishi wa Serikali atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara.

Katibu Mkuu. *Kif.34 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(2) Kutakuwa na Katibu Mkuu katika Afisi ya Rais, Katibu Mkuu katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Katibu Mkuu katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Makatibu Wakuu wengine wa Wizara mbali mbali kama Rais atakavyoona inafaa.

(3) Makatibu Wakuu waliotajwa kwenye kijifungu cha (2) cha kifungu hiki watateuliwa na Rais.

(4) Rais anaweza kuteua Naibu Katibu Mkuu wa Wizara.

(5) Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu yeyote hatoanza kazi yake mpaka kwanza aapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo chengine chochote cha utendaji wa kazi zake mbele ya Rais kama kitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

## Sehemu ya Nne

## Madaraka ya Serikali

Malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**51**. Madaraka ya Serikali ya Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Rais, na kwa mujibu wa Katiba hii, anaweza kuyatekeleza yeye mwenyewe moja kwa moja au kuwapa viongozi walio chini yake kutekeleza madaraka hayo. Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika kifungu hiki hayazuii sheria kukabidhi madaraka ya kutekeleza kazi kwa chombo chochote cha umma kwa mtu mwengine yeyote ambaye si Rais wa Zanzibar.

Kutolazimika kwa Rais kufuata ushauri wa mtu.

**52.** Rais wa Zanzibar halazimiki kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote katika utekelezaji wa shughuli zake, isipokuwa kama sheria inaagiza vyenginevyo.

Uanzishaji wa Afisi na Wadhamini wa Afisi hizo.

**53**. Kwa mujibu wa Katiba hii na bila ya kuathiri masharti ya Sura ya Nane au Sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi mamlaka:

(a) ya kuanzisha au kufuta afisi katika Zanzibar; na

(b) ya kuteua Wakuu wa afisi hizo na ya kupandisha cheo kwa muda wa utumishi, kufukuzwa na kushughulikia na hatua za kinidhamu kwa watu walioteuliwa kushika dhamana za afisi hizo,

yamo mikononi mwa Rais.

Muda wa kufanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *Kif.35 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**54**.(1) Isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo na Katiba hii au sheria yoyote nyengine kila mtu anayefanya kazi katika afisi ya Serikali ya Zanzibar atashika dhamana hiyo hadi hapo Rais atakavyoamua vyenginevyo.

(2) Katika kifungu hiki "Afisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" maana yake ni afisi ya Serikali, Idara Maalum au shughuli nyengine yoyote ilioanzishwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mujibu wa Katiba hii na inajumuisha pia afisi katika mashirika yoyote ya Serikali.

Mwanasheria Mkuu.

**55**.(1) Kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ambaye ni Mzanzibari na ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu hatafaa kuchaguliwa kuwa Mwanasheria Mkuu au kufanyakazi za Mwanasheria Mkuu mpaka awe na sifa za kumwezesha kuwa Mwanasheria katika Zanzibar na ambaye ana sifa hizo kwa muda usiopungua miaka saba.

(3) Mwanasheria Mkuu atakuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na wadhifa wake na atashika ujumbe huo mpaka uteuzi wake utakapofutwa na Rais au mara tu kabla ya Rais mteule kushika madaraka ya Rais.

Kazi za Mwanasheria Mkuu. Kif. 16 cha Sheria Nam. 2/2002.

**56**. Mwanasheria Mkuu ndiye atakayekuwa Mshauri Mkuu wa kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na atatekeleza shughuli nyengine zozote za kisheria zitazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Rais au kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria nyenginezo zozote.

Mkurugenzi wa Mashtaka. Kif. 17 cha Sheria Nam. 2/2002.

**56A-**(1)(a) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atateuliwa na Rais.

(b) Mkurugenzi wa Mashtaka atashika wadhifa wake kwa kipindi cha miaka mitano na ataweza kuteuliwa tena kwa vipindi vyengine vya miaka mitano mitano.

(2) Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka mpaka awe na sifa za kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahkama Kuu.

(3) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kufanya haya yafuatayo:

(a) kufungua na kushughulikia mashtaka yoyote ya jinai dhidi ya mtu yeyote mbele ya Mahkama yoyote (isipokuwa ya Kijeshi) kuhusiana na kosa lolote ambalo mtu huyo anashtakiwa nalo;

(b) kuchukua na kuendeleza mashtaka yoyote ya jinai ambayo mwanzoni yalifunguliwa na mtu au chombo chengine; na

(c) kusitisha mashtaka yoyote ya jinai ambayo yalianzishwa na mtu yeyote au chombo chochote.

(4) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kijifingu (3) yanaweza kutekelezwa na Mkurugenzi wa Mashtaka mwenyewe au na watu wengine kwa maagizo au amri maalum kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

(5) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya aya (b) na (c) ya kijifungu (3) yatakuwa mikononi mwake na hayataingiliwa na mtu yeyote au chombo chochote. Isipokuwa pale ambapo mtu mwengine au chombo chengine kimefungua mashtaka ya jinai, basi hakuna chochote katika kijifungu hiki kitakachozuia kufutwa kwa mashtaka hayo na mtu au chombo kilichoshtaki kwa idhini ya Mahkama.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, rufaa yoyote kutokana na hukumu katika kesi ya jinai yoyote kwenye Mahkama yoyote, au suala lolote la kisheria lilioachiwa kwa ajili ya mashtaka hayo kufikishwa kwenye Mahkama nyengine, itahesabiwa kuwa ni sehemu ya mashtaka hayo. Kwa kuzingatia kwamba yale mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kijifungu (3) (c) hayatatekelezwa kwa ajili ya rufaa yoyote ya mtu ambaye amehukumiwa katika kosa la jinai lolote kuhusiana na suala lolote la kisheria lililowekwa makusudi kwa ajili ya mtu huyo.

(7) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, Mkurugenzi wa Mashtaka hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwengine yeyote au Idara yoyote ya Serikali, lakini maelezo haya ya kifungu hiki hayatazuia Mahkama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mkurugenzi wa Mashtaka ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au siyo.

(8) Katika kutumia uwezo wake chini ya kifungu hiki, Mkurugenzi wa Mashtaka atatilia maanani umuhimu wa maslahi

ya Taifa kwa kutaka kuona haki inatekelezwa na nia yake ya kuzuia utumiaji mbaya wa vyombo vya kisheria inatimizwa.

(9) Mkurugenzi wa Mashtaka hatoweza kuondolewa ndani ya kipindi chake cha miaka mitano isipokuwa kwa sababu na utaratibu uliowekwa kuondolewa Jaji wa Mahkama Kuu kwa mujibu wa kifungu cha 95 cha Katiba hii.

(10) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kuhusu mambo yafuatayo:

(a) Mwenendo wa mashtaka kwa ujumla;

(b) Afisa au mtu mwengine yoyote mwenye sifa ambaye Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kukasimu madaraka yake;

(c) utaratibu wa kukata rufaa na muda wa kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahkama yoyote katika kesi ya jinai;

(d) utaratibu wa kuanzisha au kufungua shtaka na mtu binafsi au na taasisi za Serikali na zisizokuwa za Serikali;

(e) kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kuingilia au kujaribu kuingilia utekelezaji wa madaraka ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria yoyote.

Kiapo cha uaminifu. Kif. 18 cha Sheria Nam. 2/2002 na *Kif. 36 cha Sheria Nam.9/2010.*

**57**. Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka hatoanza kazi yake mpaka aapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo chengine cha utekelezaji wa kazi zake na Rais kama kitakavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

**58**.-(1) Rais anaweza kumteua mtu yeyote kama ni Mshauri wake Maalum ili kumsaidia katika utendaji wa kazi zake. Washauri Maalum.

(2) Uteuzi wowote chini ya kifungu hiki utafanyika kama apendavyo Rais na hautaendelea tena iwapo mtu mwengine atashika madaraka yaUrais.

**59**. Rais anaweza: Uwezo wa kutoa msamaha.

(a) kutoa msamaha bila ya masharti au kwa masharti kwa mtu yeyote aliyehukumiwa kwa kosa lolote;

(b) kutoa uahirisho ama wa muda au wa moja kwa moja katika utekelezaji wa adhabu yoyote iliyotolewa na Mahkama kwa mtu huyo kuhusiana na kosa alilotenda;

(c) kubadili adhabu aliyopewa mtu kutokana na kosa lolote na kuifanya iwe ndogo zaidi;

(d) kumsamehe kabisa au kwa kiasi fulani mtu yeyote aliyepewa adhabu kwa kosa lolote au adhabu ya utaifishaji iliyotolewa na Serikali dhidi yake.

**60**.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Ushauri kwa Rais katika uwezo wa kutoa msamaha ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao: Kamati ya Ushauri katika uwezo wa kutoa msamaha.

(a) Mwanasheria Mkuu akiwa ndiye Mwenyekiti;

(b) si chini ya wajumbe watatu na si zaidi ya wajumbe watano watakaoteuliwa na Rais, ambapo kati yao angalau mmoja atakuwa ni Waziri na angalau mmoja atakuwa ni mtu mwenye sifa za kuwa Daktari katika Zanzibar.

(2) Mjumbe wa Kamati aliyeteuliwa kwa mujibu wa kijifungu (1)(b) ataendelea na dhamana yake kwa kipindi kilichoainishwa kwenye amri iliyomteua.

Kwa kuzingatia kwamba kiti chake kitakuwa wazi:

(i) ikiwa mtu huyo alipochaguliwa ni Waziri, pale atakapoachishwa uwaziri;
(ii) ikiwa Rais ataamuru hivyo kwa maandishi.

(3) Bila ya kutegemea kasoro katika jumla ya wajumbe wote, Kamati hiyo inaweza kufanyakazi na shughuli zake hazitaathirika kwa kuwepo au kutokuwepo kwa mtu yeyote ambaye hawajibiki kuwepo au kushiriki katika Kamati hiyo.

(4) Kamati hiyo itapanga utaratibu wake wenyewe.

Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.
*Kif.37 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**61**.-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Mkoa katika kila Mkoa wa Zanzibar ataeteuliwa na Rais.

(2) Kutakuwa na Mkuu wa Wilaya katika kila Wilaya ya Zanzibar ataeteuliwa na Rais.

(3) Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya aliyeteuliwa kwa mpangilio chini ya kijifungu (1) na (2) cha kifungu hiki hatoanza kazi zake hadi kwanza aapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo cha utendaji wake wa kazi zake mbele ya Rais.

Kazi za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

**62**.-(1) Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu, kwa kadiri itavyokuwa wa Mkoa ule au Wilaya ile.

(2) Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anaweza, akipenda na bila kuathiri masharti yoyote katika Katiba hii au Sheria nyengine yoyote, kutoa madaraka yake kwa shughuli zozote za Serikali ya Mkoa huo au ya Wilaya hiyo, kwa kadiri itavyokuwa kwa mtu yeyote anayehisi anafaa, isipokuwa tu madaraka ya kuteuliwa Kaimu Mkuu wa Mkoa au Wilaya yatakuwa mikononi mwa Rais.

# SURA YA TANO

## Baraza la Wawakilishi

## Sehemu ya Kwanza
## Muundo wa Baraza la Kutunga Sheria

**63**.-(1) Kutakuwa na Baraza la Kutunga Sheria ambalo litajuilikana kama Baraza la Wawakilishi litalokuwa na sehemu mbili, Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Wawakilishi kwa upande wa pili.

Baraza la Kutunga Sheria. *Kif.39 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(2) Iwapo, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au masharti ya sheria nyengine jambo lolote linahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na sehemu zote mbili za Baraza la Kutunga Sheria, basi jambo hilo halitakuwa na nguvu za kisheria mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vile vile na Rais.

**64**. Kutakuwa na Baraza la Wawakilishi ambalo, bila ya kuathiri masharti mengine yoyote yaliyomo katika Katiba hii litakuwa na Wajumbe wafuatao:

Kuanzishwa kwa Baraza Ia Wawakil-ishi. *Kif. 40 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(a) Wajumbe wa kuchaguliwa kutokana na kifungu cha 65 cha Katiba hii;

(b) Wajumbe wa kuteuliwa kutokana na kifungu cha 66 cha Katiba hii;

(c) Wajumbe wanawake wa Baraza la Wawakilishi kutokana na kifungu cha 67 cha Katiba hii;

(d) Spika iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(e) Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kutokana na kifungu 55 (3) cha Katiba hii.

Ucha-guzi wa Wajum-be wa kuchagu-liwa.

**65**.-(1) Zanzibar itagawanywa katika majimbo ya uchaguzi kutokana na kifungu cha 120 cha Katiba na kila jimbo moja la uchaguzi litachagua mtu mmoja kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa njia ambayo itaelezwa na Katiba au chini ya sheria nyengine yoyote.

(2) Kila mtu ambaye amejiandikisha katika jimbo la uchaguzi kama ni mpiga kura wa kumchagua Mjumbe, isipokuwa awe amewekwa kizuizini kwa njia ya halali au hafai kutokana na sheria, kupiga kura katika uchaguzi huo kwa njia ambayo amekutikana na kosa lenye kuhusiana na uchaguzi au kwa njia ambayo imeripotiwa kuwa amepatikana na kosa hilo katika Mahkama au kujaribu kubatilisha uchaguzi, atastahiki kupiga kura katika jimbo la uchaguzi hilo kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

(3) Uandikishaji wa kupiga kura wa Wajumbe wa kuchaguliwa na uendeshaji wa uchaguzi huo utaongozwa na kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi.

Wajumbe wa kuteu-liwa.
*Kif. 41 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**66**. Kutakuwa na Wajumbe kumi wa kuteuliwa wa Baraza la Wawakilishi ambao watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoelezwa na kifungu cha 68(a) na (c) cha Katiba ambao wakiteuliwa watafaa kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

*Kif. 3 cah Sheria Nam. 8/2016*

Isipokuwa kwamba Wajumbe wasiopungua wawili watateuliwa na Rais kwa kushauriana na Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi au kwa kushauriana na Vyama vya Siasa iwapo hakuna Kiongozi wa Upinzani.

**67**.-(1) Kutakuwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawake kwa idadi ya asilimia arobaini (40%) ya wajumbe wote wa kuchaguliwa katika majimbo ya uchaguzi ambao ni Wazanzibari na ambao watapendekezwa na vyama vya siasa vinavyowakilishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki.

Wajumbe Wanawake katika Baraza. *Kif. 20 cha Sheria Nam. 2/2002 na Kif.42 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(2) Kila chama cha siasa kitachoshinda zaidi ya asilimia kumi (10%) ya viti vya majimbo katika Baraza la Wawakilishi kitapendekeza idadi ya majina ya wanachama wanawake kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa uwakilishi baina ya vyama vya siasa vilivyoshinda uchaguzi katika majimbo na kupata viti katika Baraza la Wawakilishi na kupeleka majina na sifa zao kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(3) Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar baada ya kuridhika kuwa mwanamke aliyependekezwa ana sifa za kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 68 cha Katiba hii, itamtangaza mara moja mwanamke huyo kuwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Isipokuwa kwamba ieleweke kuwa katika kufanya hesabu ya idadi ya Wajumbe wa kila chama cha siasa kila sehemu iliyozidi nusu ya Mjumbe itachukuliwa kuwa ni Mjumbe kamili.

**68.** Mtu atafaa kuchaguliwa kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa, na hatofaa kuchaguliwa mpaka, siku ya kuchaguliwa kwake katika uchaguzi:

Sifa za kuchaguliwa. *Kif. 21 cha Sheria Nam. 2/2002.*

(a) awe ni Mzanzibari aliyetimia umri wa miaka ishirini na moja;

(b) awe amejiandikisha au ana sifa za kujiandikisha katika jimbo la uchaguzi kama mpiga kura katika uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi;

(c) awe anaweza kusoma na isipokuwa hana uwezo wa kuona au magonjwa mengine ya kiwiliwili, anasema lugha ya Kiswahili;

(d) awe ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa kilichosajiliwa rasmi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya 1992;

(e) awe ni mtu ambaye hakuzuiliwa kugombea uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki au kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Kutofaa kuchaguliwa.
*Kif. 22 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**69**.-(1) Hakuna mtu atakayechaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa mtu huyo:

(a) ana uraia wa nchi nyengine; au

(b) Mahkama Kuu imeamua, baada ya kushauriwa na Daktari Bingwa wa magonjwa ya akili, kuwa ana ugonjwa wa akili; au

(c) si mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama; au

(d) ametiwa hatiani na kupelekwa Chuo cha Mafunzo au Gereza la Tanzania Bara kwa kosa la jinai kwa kipindi cha kuanzia miezi 6 na zaidi au kosa la uchaguzi linalohusu uaminifu ndani ya miaka mitano kabla ya uchaguzi.

(2) Mtu hawezi kugombea kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa wakati huo yeye ni Mweyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(3) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (d) ya kijifungu (1) ya kifungu hiki, yaani:

(a) ikiwa mtu amepata adhabu mbili au zaidi kufungwa muda wa mfululizo, basi adhabu hizo zitahisabiwa kuwa ni adhabu mbali mbali iwapo muda uliotajwa katika moja ya adhabu hizo hauzidi miezi sita, lakini iwapo muda uliotajwa katika adhabu yoyote kati ya adhabu hizo unazidi miezi sita basi adhabu hizo zote zitahesabiwa kama ni adhabu moja;

(b) ikiwa mtu amepewa adhabu ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au Gerezani akifahamika kuwa adhabu hiyo ya kufungwa imetolewa badala ya adhabu ya kutozwa faini au imetolewa kwa sababu mtu huyo ameshindwa kulipa faini aliyoamrishwa kulipa, basi muda wa kifungo cha namna hiyo hautahesabiwa.

(4) Kwa ajili ya ufafanuzi wa maelezo kuhusu sifa za uchaguzi yaliyomo katika vifungu vifuatavyo, kila itakapotajwa chini ya Katiba hii kwamba utekelezaji wa jambo lolote, sifa za uongozi, basi ila za uongozi au mtu ambaye hakupoteza sifa za uongozi, basi ila iwapo maelezo yanahitajia vyenginevyo, ifahamike kuwa sifa zinazohusika ni zile zinazomwezesha mtu kuchaguliwa kuwa Mjumbe Mwakilishi au Baraza la Mapinduzi kama viongozi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyoelezwa katika vifungu mbali mbali vya Katiba hii miongoni mwao ikiwa:

(a) ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka aliyopewa kwa ajili ya manufaa yake binafsi, au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa madaraka hayo;

(b) ni mwiko kwa kiongozi kupokea kipato cha kificho, au rushwa au kushiriki katika mambo yoyote ya magendo; na

(c) kiongozi aliyeachishwa uongozi hatakuwa na haki ya kuomba tena nafasi ya uongozi mpaka ipite miaka mitano.

Kiapo cha Mjumbe Mwakilishi.

**70**. Kila Mjumbe Mwakilishi atatakiwa kuapishwa, katika Baraza la Wawakilishi, kiapo cha uaminifu kama kitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi lakini Mjumbe Mwakilishi anaweza kushiriki katika uchaguzi wa Spika, hata kabla hajaapishwa.

Muda wa Wajumbe kushika madaraka yao.
*Kif. 9 cha Sheria Nam. 13/1992 na Kif. 23 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**71**.-(1) Mjumbe Mwakilishi ataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi na ataacha kiti chake katika Baraza la Wawakilishi litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Mjumbe Mwakilishi ingemfanya mtu asiwe na sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi au apoteze sifa za Uongozi;

(b) ikiwa Mjumbe Mwakilishi huyo atachagu1iwa kuwa Rais wa Zanzibar;

(c) ikiwa Mjumbe Mwakilishi atakosa kuhudhuria Mikutano ya Baraza mitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Spika;

(d) baada ya Baraza la Wawakilishi kuvunjwa;

(e) iwapo Mahkama Kuu itaamuru Mjumbe apoteze kiti chake kwa mujibu wa kifungu cha 72 cha Katiba hii;

(f) ikiwa Mjumbe, kwa maandishi yake na ayatume kwa Spika atajiuzulu kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(g) Mjumbe akijiondoa uanachama katika chama chake kilichompendekeza kuwa mgombea.

(2) Spika wa Baraza la Wawakilishi atatoa taarifa rasmi kwa Baraza na kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuhusu kiti cha Mjumbe Mwakilishi kuwa wazi katika kutekeleza masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatayomwezesha Mjumbe Mwakilishi kukata rufaa kwa mujibu wa Sheria kupinga hukumu ya kuthibitishwa kwake kuwa ni mtu mwenye ugonjwa wa akili au kupinga adhabu ya kifo au ya kufungwa Chuo Cha Mafunzo au Gerezani, na Sheria hiyo inaweza kueleza kwamba hiyo hukumu inayopingwa na huyo Mjumbe Mwakilishi haitatiliwa nguvu kisheria mpaka umalizike kwanza muda utakaotajwa katika Sheria hiyo.

Uamuzi wa suala kama mtu ni mjumbe Mwakilishi ama sio.
*Kif. 10 Sheria Nam. 13/1992.*
*Kif. 43 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**72**.-(1) Mahkama Kuu ya Zanzibar ndio pekee yenye mamlaka na uwezo wa kusikiliza na kuamua mashauri yote yanayohusiana na uchaguzi wa Zanzibar.

(2) Wakati wa kusikiliza shauri lolote chini ya kifungu hiki, Jaji anaweza kuteua washauri wawili wa Mahkama kwa kumsaidia.

Spika.
*Kif. 11 Sheria Nam. 13/1992. Kif.44 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**73**.-(1) Kutakuwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye atachaguliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa watu ambao ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au mwenye sifa za kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri au mtu mwenye madaraka ya aina nyengine yoyote yatayotajwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya kifungu hiki, hataweza kuchaguliwa kuwa Spika.

(3) Spika ataacha kuwa Spika na ataacha kiti cha Spika litakapotokea lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) iwapo mtu huyo alichaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi basi ikiwa ataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa sababu yoyote ambayo haihusiki na kuvunjwa Baraza la Wawakilishi; au

(b) ikiwa kutatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Spika lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi au apoteze sifa za uchaguzi wa Spika; au

(c) ikiwa mtu huyo ataondolewa kwenye madaraka ya Spika kwa Azimio la Baraza la Wawakilishi lililoungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote.

(4) Hakuna shughuli itakayotekelezwa katika Baraza la Wawakilishi (isipokuwa uchaguzi wa Spika) wakati wowote ambao

kiti cha Spika kitakuwa wazi, lakini kijifungu hiki, hakitozuwia Kamati za Baraza la Wawakilishi kufanya shughuli zao.

(5) Mtu yeyote ambaye si Mjumbe Mwakilishi, atayechaguliwa kuwa Spika, atatakiwa, kabla ya kuanza kutekeleza madaraka yake kuapishwa katika Baraza la Wawakilishi kiapo cha uaminifu.

Naibu Spika. *Kif.45 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**74**.-(1) Kutakuwa na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye atachaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutokana na Kanuni za Baraza ambaye atakuwa ni Mjumbe Mwakilishi ambaye hatokuwa Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi.

(2) Baraza la Wawakilishi litachagua Naibu Spika:

(a) chini ya masharti ya kifungu cha 73(4) katika mkutano wake wa mwanzo baada ya kuvunjwa Baraza; na

(b) litakapokutana Baraza kwa mara ya mwanzo wakati kiti cha Naibu Spika kiwazi kwa njia ambayo sio sababu ya kuvunjwa kwa Baraza, au kwa haraka iwezekanavyo.

(3) Kiti cha Naibu Spika kitakuwa wazi:

(a) ikiwa Baraza la Wawakilishi ni mara yake ya mwanzo kukutana toka kuvunjwa kwa Baraza lililopita;

(b) ikiwa amechaguliwa kuwa Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Mkoa au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi;

(c) ikiwa amesita kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa njia ambayo sio kwa kuvunjwa Baraza; au

(d) ikiwa Baraza la Wawakilishi limeamua kwa uamuzi wa kura zisizopungua theluthi mbili za Wajumbe wote kuwa Naibu Spika huyo aondolewe katika kiti hicho.

Taratibu za uchaguzi wa Spika na Naibu Spika.

**75**. Katika Uchaguzi wowote wa Spika au Naibu Spika kura za Wajumbe wa Baraza zitakuwa za siri.

Katibu wa Baraza la Wawakil-ishi.

**76**.-(1) Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi atakayeteuliwa na Rais.

(2) Afisi ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi na Afisi za wafanyakazi wake zitakuwa ni Afisi katika huduma ya Serikali.

(3) Katibu wa Baraza la Wawakilishi hatoanza kazi yake ila kwanza ale kiapo cha uaminifu na kiapo chengine chochote kitachowekwa na sheria.

Afisi ya Baraza la Wawakil-ishi.
*Kif. 6 cha Sheria Nam 11/1995.*

**77**.-(1) Kutakuwa na Afisi ya Baraza la Wawakilishi itayoongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi na itakuwa na nafasi za madaraka kama itavyoidhinishwa na Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi ambayo itakuwa na uwezo wa kuajiri maafisa na watumishi wote wa Baraza, kuwapandisha vyeo, kuwachukulia hatua za kinidhamu na kufanyakazi nyengine zozote zitazoelezwa na Sheria kuhusu Utumishi katika Afisi ya Baraza, isipokuwa kwamba Katibu wa Baraza la Wawakilishi atateuliwa na Rais kwa mujibu wa kifungu cha 76 cha Katiba.

(3) Muundo na taratibu za Tume ya Utumishi wa Baraza utakuwa kama itavyoelezwa na Sheria itayotungwa kwa madhumuni hayo.

(4) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria ya kuweka mfumo wa utawala na uendeshaji na mambo mengine yanayohusu Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

## Sehemu ya Pili

## Sheria na Taratibu Katika Baraza la Wawakilishi

**78**.-(1) Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

Nguvu za kutunga Sheria. *Kif.46 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(2) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, nguvu za kutunga sheria katika Baraza la Wawakilishi itakuwa kwa kupitishwa Miswada katika Baraza la Wawakilishi.

(3) Wakati Mswada umepitishwa na Baraza la Wawakilishi, Spika ataupeleka kwa Rais ndani ya siku thelathini kupata kibali chake.

(4) Iwapo Mswada ambao umepitishwa na Baraza la Wawakilishi umepelekwa kwa Rais wa Zanzibar kwa kupata kibali hicho, utakuwa sheria na hivyo utachapishwa katika Gazeti Rasmi.

(5) Baraza la Wawakilishi linaweza kuahirisha kuanza kutumika kwa sheria iliyotungwa na bila kuathiri masharti ya kifungu cha 12 cha Katiba hii linaweza kufanya sheria kuanza siku za nyuma.

(6) Sheria inayotungwa na Baraza la Wawakilishi itajulikana kuwa ni "Sheria ya Baraza la Wawakilishi" na jina la utunzi litakuwa "Imetungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar".

Utaratibu wa kutunga Sheria.
*Kif.47 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**79**.-(1) Baada ya Mswada kuwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake, Rais anaweza ndani ya kipindi cha siku tisini ama kukubali au kukataa kuukubali, na iwapo atakataa kuukubali Mswada, basi ataurudisha kwenye Baraza la Wawakilishi pamoja na maelezo ya sababu zake za kukataa kuukubali Mswada huo.

*Kif.4 cha Sheria Nam. 8/2016.*

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 78(4) cha Katiba mara baada ya siku tisini tokea siku ya kuwasilishwa Mswada kwa Rais kumalizika bila ya kukubaliwa au kukataliwa na Rais, Mswada huo utachukuliwa kuwa ni Sheria.

(3) Endapo itatokea Mswada kuwa Sheria chini masharti ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, Spika ataweka maelezo katika Sheria hiyo kuonesha kuwa Sheria hiyo imekuwa Sheria kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 79(2) cha Katiba.

(4) Baada ya Mswada kurudishwa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Masharti ya kifungu hiki, hauwezi kupelekwa tena kwa ajili ya kupata kibali chake kabla ya kumaliza muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, isipokuwa kama katika hatua yake ya mwisho kwenye Baraza la Wawakilishi kabla haujapelekwa tena kwa Rais Mswada huo umeungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote.

(5) Iwapo Mswada umerudishwa kwenye Baraza la Wawakilishi na Rais halafu ukaungwa mkono kwenye Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote kama ilivyoelezwa katika kijifungu cha (2) na kupelekwa kwa Rais, kwa ajili ya kupata kibali chake kwa mara ya pili kabla haujamalizika muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, basi atatakiwa kuukubali Mswada huo kabla ya kumalizika muda wa siku ishirini na moja tangu Mswada huo ulipowasilishwa kwake la sivyo basi itabidi alivunje Baraza la Wawakilishi.

(6) Masharti yaliyomo katika kijifungu hiki au katika kifungu cha 79(1) cha Katiba hii hayatalizuia Baraza la Wawakilishi kutunga sheria ya kuweka masharti ambayo yanaweza kukabidhi kwa mtu yeyote kwa Idara yoyote ya Serikali madaraka ya kuweka kanuni zenye nguvu za kisheria au kuzipa nguvu za kisheria kanuni zozote zilizowekwa na mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali.

Kubadilisha Katiba.

**80.-**(1) Kwa masharti ya kifungu hiki Baraza la Wawakilishi linaweza kubadilisha kifungu chochote katika Katiba hii.

(2) Mswada wa Baraza la Wawakilishi wa kubadilisha Katiba hii hautopitishwa na Baraza isipokuwa uwe umeungwa mkono kwa mara ya kwanza na mara ya pili katika kusomwa kwa kura si chini ya theluthi mbili ya kura zote za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(3) Katika kifungu hiki:

(a) marejeo katika Katiba hii ni marejeo katika Katiba kama itakavyorekebishwa mara kwa mara;

(b) marejeo ya kubadilisha Katiba hii ni marejeo ya kufanya marekebisho, masahihisho au kutunga ikiwa na mabadiliko au masahihisho katika kifungu chochote cha Katiba hii, kusimamisha au kufuta kifungu hicho na utungaji wa kifungu tofauti katika mahala pa kifungu cha zamani.

Kura ya maoni kwa mabadiliko ya baadhi ya vifungu vya Katiba. *Kif.48 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**80A-**(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 80 cha Katiba, Baraza la Wawakilishi halitaweza kufanya mabadiliko ya Katiba kuhusiana na sharti lolote liliomo katika kifungu chochote kilichoainishwa katika kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, mpaka kwanza mabadiliko hayo yakubaliwe na wananchi kwa Kura ya Maoni.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, vifungu vinavyohitaji Kura ya Maoni ni:

(a) vifungu vyote vya Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Kwanza;

(b) kifungu cha 9;

(c) vifungu vyote vya Sura ya Tatu;

(d) kifungu cha 26;

(e) kifungu cha 28;

(f) vifungu vyote vya Sehemu ya Pili na Sehemu ya Tatu ya Sura ya Nne isipokuwa kifungu cha 49 na 50;

(g) kifungu cha 80A; na

(h) vifungu vya 121(1) na 123 vya Sura ya Kumi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya vijifungu vya (1) na (2) vya kifungu hiki, kifungu chochote kilichotajwa chini ya kijifungu cha (2) kinaweza kurekebishwa bila kuitisha Kura ya Maoni pale Baraza la Wawakilishi kwa Azimio Maalum lililopitishwa kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wajumbe waliohudhuria na kupiga kura, litaporidhika kwamba marekebisho yanayotaka kufanywa ni ya kiutaratibu, ya kiuandishi ama ya kuweka bayana jambo lenye utatanishi na hayaathiri madhumuni ya msingi ya kifungu husika.

(4) Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, Kura ya Maoni inaweza kuitishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

**81.** Ki1a Kikao cha Baraza la Wawakilishi kitaongozwa na:

Uongozi wa kikao cha Baraza la Wawakilishi. *Kif.49 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(a) Spika; au

(b) ikiwa hayupo Naibu Spika; au

(c) ikiwa Spika hayupo na Naibu Spika hayupo, Mjumbe mwengine wa Baraza la Wawakilishi (asiyekuwa Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi) kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakayemchagua kwa ajili hiyo.

**82**.-(1) Baraza la Wawakilishi linaweza kuendesha shughuli bila ya kujali kuweko kwa kiti wazi kuhusu Mjumbe kuhusiana na kiti ambacho hakikujazwa wakati Baraza ndio kwanza liitishwe au kuundwa kwa mara ya kwanza na shughuli hizo zitaendelea bila ya kujali kuweko kwa mtu asiyehusika kuwepo au kupiga kura katika Baraza au kuwepo katika shughuli zinazoendelea.

Viti vilivyo wazi katika Baraza la Wawakilishi na utaratibu wa kuendesha shughuli za Baraza.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika kifungu cha 80 cha Katiba hii, idadi ya Wajumbe kufanya mkutano itakuwa nusu ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi.

**83**.-(1) Isipokuwa kama imeelezwa vyengine katika Katiba hii, suala lolote au uamuzi katika Baraza la Wawakilishi litaamuliwa kutokana na idadi kubwa ya Wajumbe waliohudhuria kwenye kikao na kupiga kura.

Upigaji kura katika Baraza la Wawakilishi.

(2) Jambo lolote litakalopelekwa kwa uamuzi katika Baraza la Wawakilishi, mtu atakayekuwa anaongoza kikao cha Baraza la Wawakilishi:

(a) ikiwa ni Spika, atakuwa na kura ya uamuzi na siyo kura ya asili;

(b) ikiwa siye Spika atakuwa na kura ya uamuzi pamoja na kura ya asili;

(3) Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinaweza kuweka vifungu ambavyo Mjumbe ambaye anapiga kura na huku akiwa na maslahi fulani ya jambo linalopigiwa kura asiwe na kura.

Madaraka ya Rais katika Baraza la Wawakilishi. *Kif.50 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**84**. Rais atahusika katika mamlaka ya shughuli zake kama Rais wa Zanzibar kuhutubia Baraza la Wawakilishi wakati atakaoona unafaa kufanya hivyo.

Kamati za Baraza la Wawakil-ishi *Kif. 7 cha Sheria Nam 11/1995.*

**85**.(1) Kutakuwa na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zitazoundwa kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki cha Katiba hii, kazi na shughuli za Kamati za Baraza la Wawakilishi zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

(3) Baraza linaweza Iikaanzisha Kamati nyengine zozote inazohisi zinafaa.

Baraza kutunga Sheria. *Kif.51 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**86.-**(1) Baraza la Wawakilishi linaweza, kwa ajili ya ufanisi mzuri wa kazi zake, kutunga sheria kuhusiana na haki za Wajumbe, nguvu zao, fursa na kinga zao pamoja na Kamati zao kwa misingi inayokubalika.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, Baraza la Wawakilishi linaweza kufanya Kanuni za kudumu za Baraza hilo zikitilia maanani amri za kuendesha mikutano, na kwa kutilia maanani sheria zitazotungwa kwa mujibu wa kijifungu (1) cha kifungu hiki kutoka katika kanuni hizo haki za Wajumbe, nguvu zao, fursa na kinga za Wajumbe wa Kamati zao.

(3) Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza majukumu yao Barazani, katika Kamati za kudumu za Baraza au katika Kamati teule za kudumu za Baraza:

(i) watakuwa na kinga kwa mashtaka yoyote ya jinai au madai;

(ii) watakuwa na kinga ya maelezo wanayoyazungumza; na

(iii) hawatokamatwa wakati wakiwa katika shughuli hizo.

**87**.-(1) Bila ya kuathiri kifungu hiki, lugha rasmi ya Baraza la Wawakilishi itakuwa ni Kiswahili. Lugha rasmi.

(2) Kila Mswada (pamoja na vijalizo vilivyofuatana na Mswada), kila sheria inayotungwa na Baraza, kila Sheria ya msingi au sheria inayopendekezwa chini ya chombo cha sheria na Baraza, maafikiano yote ya kifedha na nyaraka zenye kuhusiana na kila sheria halisi au inayopendekezwa, kusahihishwa au inayoendelea itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili na ikihitajika kwa lugha ya Kiingereza.

**88.** Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na vifungu vya Katiba hii, litafanya kazi kwa mambo yafuatayo ya utekelezaji: Kazi za Baraza la Wawakilishi.

(a) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo;

(b) kujadili shugliuli za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka wa Bajeti katika Baraza la Wawakilishi;

(c) kuuliza masuala mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi;

(d) kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya Serikali katika njia ile ile ambayo Bajeti ya mwaka inaidhinishwa.

## Sehemu ya Tatu

## Kuitisha na Kuvunja Baraza la Wawakilishi

Kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi
*Kif. 24 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**89**.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, mkutano wa Baraza utakuwa sehemu yoyote katika Zanzibar na utafanyika wakati wowote ambapo Rais ataamuru.

(2) Kutakuwa na mkutano wa Baraza la Wawakilishi angalau mara moja kila mwaka na kipindi cha miezi kumi na mbili hakitopita baina ya mkutano mmoja na mwingine.

Uchaguzi Mkuu na Mkutano wa mwanzo.
*Kif. 25 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**90**.-(1) Wakati Baraza litakapovunjwa, Uchaguzi Mkuu wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi utafanywa na mkutano wa mwanzo wa Baraza jipya utafanywa si zaidi ya siku tisini toka kuvunjwa kwa Baraza.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, kikao cha Baraza la Wawakilishi katika mkutano wowote wa Baraza utafanyika wakati wowote na siku yoyote kama itakavyoelezwa kulingana na Kanuni za Baraza.

(3) Kukitokea hali ya hatari au kama kuna hali ya hatari ambayo Rais anaona inasababisha kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi na iwapo wakati huo Baraza la Wawakilishi limevunjwa na matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu

hayajatangazwa basi Rais aweza kutoa Taarifa Maalum ya kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi na kuagiza kwamba Spika na watu wote waliokuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mara tu kabla ya Baraza la Wawakilishi halijavunjwa wahudhurie Mkutano huo na watahesabiwa hivyo mpaka usiku wa manane wa siku yatakapotangazwa matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu.

Kuitisha na kuvunja Baraza la Wawakilishi. *Kif. 8 cha Sheria Nam 11/1995 na Kif.52 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**91**.-(1) Rais wakati wowote anaweza kuitisha Baraza la Wawakilishi kuendelea na shughuli zake.

(2) Rais hatakuwa na uwezo wakati wowote wa kulivunja Baraza la Wawakilishi isipokuwa tu:

(a) kama Baraza la Wawakilishi limemaliza uhai wake kwa mujibu wa kifungu cha 92 cha Katiba; au

(b) anaweza kulivunja wakati wowote ndani ya miezi kumi na mbili ya mwisho ya uhai wa Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya kuitisha Uchaguzi mapema kidogo; au

(c) kama Baraza la Wawakilishi limekataa kupitisha Bajeti inayopendekezwa na Serikali; au

(d) kama Baraza la Wawakilishi limekataa kupitisha Mswada wa Sheria kwa mujibu wa kifungu cha 79 cha Katiba; au

(e) kama Baraza la Wawakilishi limekataa kupitisha hoja ambayo ni ya msingi katika sera za Serikali na Rais anaona kwamba njia muafaka ya kulinda maslahi ya Taifa si kuvunja Baraza la Mawaziri au kuteua Makamo wa Pili wa Rais mpya bali ni kuitisha Uchaguzi Mkuu; au

(f) endapo, kutokana na uwiano wa uwakilishi wa Vyama vya Siasa katika Baraza la Wawakilishi, Rais anahisi kwamba hakuna uhalali kwa Serikali iliyopo kuendelea kuwapo na wala haiwezekani kuunda Serikali mpya.

Isipokuwa kwamba hataweza kulivunja Baraza chini ya masharti ya vijifungu (b), (c), (e) na (f), kama Spika amepokea taarifa rasmi inayopendekeza kuundwa kwa Kamati Maalum ya Uchunguzi kwa madhumuni ya kumuondoa Rais madarakani kwa mujibu wa kifungu cha 37 cha Katiba.

(3) Bila ya kuathiri masharti yoyote ya Katiba, Spika anaweza wakati wowote kuliitisha Baraza la Wawakilishi kwa jambo la dharura baada ya kupata ombi la Mjumbe wa Baraza na Spika akaridhika kwamba sababu zilizoelezwa katika ombi hilo ni za msingi na inafaa Baraza la Wawakilishi kuitishwa.

Maisha ya Baraza la Wawakilishi. *Kif. 26 cha Sheria Nam. 2/2002 na Kif.53 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**92**.-(1) Maisha ya Baraza la Wawakilishi yataendelea kwa muda wa miaka mitano tangu tarehe ile ulipoitishwa Mkutano wake wa kwanza baada ya kuundwa, ila tu pale iwapo Baraza la Wawakilishi limevunjwa mapema kutokana na sababu mbali mbali zilizoelezwa katika Katiba hii.

(2) Wakati wote Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakapokuwa iko kwenye vita, Baraza la Wawakilishi laweza mara kwa mara kuongeza kipindi cha miaka mitano iliyoelezwa katika kijifungu cha (1) cha kifungu hiki na si zaidi ya miezi sita kwa wakati mmoja.

# SURA YA SITA

## Sheria

### Sehemu ya Kwanza

### Mahkama Kuu

**93**.-(1) Kutakuwa na Mahkama Kuu ya Zanzibar ambayo itakuwa ndio Mahkama ya kumbukumbu na kuwa na mamlaka yote ya kesi za jinai na madai na nguvu nyengine zitazopewa kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria nyengine yoyote.

Kuundwa kwa Mahkama Kuu.

(2) Majaji wa Mahkama Kuu watakuwa Jaji Mkuu na Majaji wengine, wasiopungua wawili wataojulikana kama Majaji wa Mahkama Kuu.

(3) Mahkama Kuu itakuwa imekamilika kisheria licha ya kuwa na nafasi wazi ya kiti cha Jaji wa Mahkama hiyo.

(4) Kazi ya Jaji haitafutwa wakati yupo mtu aliyehusika na madaraka ya kiti cha Jaji.

(5) Mahkama Kuu itakaa pahala popote ambapo Jaji Mkuu atakapoteua kwa ajili hiyo.

**94**.-(1) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama.

Uteuzi wa Majaji wa Mahkama Kuu. *Kif. 27 cha Sheria Nam. 2/2002.*

(2) Majaji wa Mahkama Kuu watateuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi ya Mahkama.

(3) Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Jaji au Kaimu Jaji wa Mahkama Kuu mpaka:

(a) awe na shahada ya Sheria ya Chuo Kikuu kinachotambuliwa au Chuo cha aina hiyo; na

(b) (i) awe au amewahi kuwa Jaji wa Mahkama zilizofanana na hii kwa kesi zote za jinai na madai katika Tanzania au sehemu yoyote ya Jumuiya ya Madola au Mahkama yenye mamlaka ya Rufaa kutoka Mahkama hizo; au

(ii) awe ni Mwanasheria wa Zanzibar au Tanzania kwa kipindi kisichopungua miaka saba; au

(iii) awe na uzoefu wa (i) na (ii) kwa pamoja usiopungua miaka saba.

(4) Ikitokea kwamba kiti cha Jaji kitakuwa wazi au kwamba Jaji Mkuu atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, basi kazi hizo zitatekelezwa na Jaji mmoja wapo atakayeteuliwa na Rais wa Zanzibar kwa ajili hiyo kama Kaimu Jaji Mkuu na Jaji huyo atatekeleza kazi hizo mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwengine na kushika madaraka ya kiti cha Jaji Mkuu au mpaka Jaji Mkuu mwenyewe ambaye alikuwa hamudu kazi zake atakaporejea kazini.

(5) Ikiwa Jaji wa Mahkama Kuu ameteuliwa kuwa Kaimu Jaji Mkuu au kwa sababu nyengine yoyote ile hawezi kufanya kazi zake za Ujaji au ikiwa Jaji Mkuu atamshauri Rais kwamba kwa hali ilivyo Mahkama Kuu inahitajia Jaji mwengine, Rais akishauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama, anaweza kumteua mtu yeyote kuwa Jaji wa Mahkama Kuu bila ya kujali umri ulioelezewa katika kifungu cha 95(1) cha Katiba hii.

(6)(a)Rais anaweza kumteua mtu yeyote kuwa Kaimu Jaji wa Mahkama Kuu kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au Jaji kwa mkataba wa kipindi maalum kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi ya Mahkama.

(b) Masharti ya kazi, marupurupu na kiinua mgongo cha Jaji kwa mkataba wa kipindi maalum yataamuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama.

(7) Mtu yeyote aliyeteuliwa chini ya kijifungu cha (5) kushikilia nafasi ya Jaji wa Mahkama Kuu, ataendelea bila kuathiri matakwa ya vijifungu (4) na (6) vya kifungu cha 95, kushika wadhifa huo hadi hapo uteuzi wake utapofutwa na Rais kutokana na ushauri wa Turne ya Utumishi ya Mahkama na ataendelea kushikilia wadhifa huo kwa muda utaokuwa muafaka kwa kutoa hukumu au kufanya kitu chengine chochote kutokana na mambo ambayo yamefanyika mbele yake.

(8) Jaji Mkuu hatoweza kuondolewa kwenye kiti cha Jaji Mkuu isipokuwa kwa sababu na utaratibu uliowekwa kuondolewa Jaji wa Mahkama Kuu kwa mujibu wa kifungu cha 95 cha Katiba hii.

Muda wa kushika madaraka ya Ujaji. *Kif. 28 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**95**.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, Jaji wa Mahkama Kuu ataendelea kushika wadhifa wake hadi kufikia umri wa miaka sitini ambapo anaweza kustaafu kwa hiari ama kuendelea hadi kufikia umri wa miaka sitini na tano ambapo atastaafu kwa lazima.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, Rais kwa kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama anaweza kumteua tena Jaji aliyekwisha staafu kushika madaraka ya Jaji wa Mahkama Kuu kwa muda au kwa ajili ya kesi maalum.

(3) Licha ya kuwa Jaji amefika umri ulioainishwa katika kijifungu cha (1) hapo juu, Jaji wa Mahkama Kuu ataendelea katika wadhifa wake huo hata baada ya kufikia umri huo mpaka pale atapomaliza shughuli zote ambazo zilimfika yeye kabla ya kutimiza umri huo.

(4) Jaji wa Mahkama Kuu ya Zanzibar aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi ya Jaji kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na sababu nyengine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(5) Jaji wa Mahkama Kuu ataondolewa kazini na Rais ikiwa suala la kuondolewa kwake limepelekwa kwa Tume iliyoundwa kwa madhumuni hayo chini ya kijifungu cha (6) cha kifungu hiki; na Tume hiyo imependekeza kwa Rais kwamba Jaji huyo anafaa kuondolewa kutokana na kutomudu kazi zake au kutokana na tabia zake mbaya.

(6) Iwapo Rais anaona kwamba suala la kumuondoa Jaji Mkuu kazini linahitaji kuchunguzwa, au iwapo Jaji Mkuu atapeleka kwa Rais kwamba suala la kumuondoa Jaji linahitaji kuchunguzwa:

(a) Rais atateua Mwenyekiti na Wajumbe wawili ambao ni Majaji au watu waliopata kuwa Majaji wa Mahkama Kuu ya Zanzibar au ya Jamhuri ya Muungano au Mahkama ya Rufaa ya kesi za Mahkama hizo.

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais wa Zanzibar kuhusu maelezo ya shauri lote na itamshauri Rais wa Zanzibar kama huyo Jaji anayehusika aondolewe kazini kwa

mujibu wa masharti ya kifungu hiki kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyengine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(7) Ikiwa suala la kumuwondoa Jaji kazini limepelekwa kwenye Tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, Rais akishauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama kwa suala la Jaji wa Mahkama Kuu, au kwa pendekezo lake mwenyewe kwa suala la Jaji Mkuu, anaweza kumsimamisha kazi Jaji huyo anayehusika na kusimamishwa kazi huko kunaweza wakati wowote kutenguliwa kwa mpango ule ule ulioelezwa wakati wa kusimamishwa kazi na kwa vyovyote vile uamuzi huo wa kusimamishwa kazi utakuwa hauna nguvu yoyote pale Tume itapopendekeza kwamba Jaji huyo asingestahili kuondolewa kazini.

(8) Jaji Mkuu au Jaji wa Mahkama Kuu hatateuliwa au kuchaguliwa kufanya kazi nyengine katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au sehemu nyengine yoyote kwa kipindi chochote kile bila ya ridhaa yake kwa maandishi.

Viapo kwa Majaji wa Mahkama Kuu.
*Kif. 54 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**96**. Jaji Mkuu, Kaimu Jaji Mkuu na Jaji wa Mahkama Kuu hatoanza kazi zake mpaka kwanza aapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo chengine chochote mbele ya Rais kitachowekwa na Sheria kwa ajili hiyo.

Uanacha-ma katika vyama vya siasa
*Kif. 9 cha Sheria Nam 11/1995.*

**97**. Itakuwa ni marufuku kwa Jaji wa Mahkama Kuu (pamoja na Jaji Mkuu), Mahakimu wa ngazi zote, Mrajis, Kaimu Mrajis, Naibu Mrajis na Msaidizi Mrajis na Makadhi wote (pamoja na Kadhi Mkuu) kujiunga na Chama chochote cha Siasa isipokuwa tu kwamba atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika kifungu cha 7 cha Katiba hii.

## Sehemu ya Pili

## Mahkama ya Rufaa

*Kif. 29 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**98**. [Kimefutwa].

Kazi na uwezo wa Mahkama ya Rufaa. *Kif. 30 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**99**. Mahkama ya Rufaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na uwezo wa kusikiliza rufaa kutoka Mahkama Kuu ya Zanzibar isipokuwa kesi zozote zinazohusika na:

(a) tafsiri ya Katiba hii;

(b) mambo ya Kiislamu ambayo yameanzia katika Mahkama za Kadhi;

(c) mambo mengine yoyote yaliyoainishwa katika Katiba hii na Sheria nyengine yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Ufafanuzi wa Katiba kupelekwa Mahkama Kuu. *Kif..31 cha Sheria Nam. 2/2002. na kif. 55 cha Sheria Nam.9/2010.*

**99A-**(1) Iwapo katika shauri lolote katika Mahkama yoyote iliyo chini ya Mahkama Kuu suala la tafsiri ya Katiba hii litajitokeza, suala hilo mara moja litawasilishwa Mahkama Kuu kwa uamuzi na shauri hilo halitaendelea mpaka uamuzi wa Mahkama Kuu uwe umepatikana.

(2) Rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahkama Kuu juu ya suala la tafsiri ya Katiba hii itasikilizwa na Mahkama Kuu mbele ya Majaji watatu bila ya kumjumuisha Jaji aliyeamua suala hilo mara ya kwanza. Majaji hao watatu watateuliwa na Jaji Mkuu.

## Sehemu ya Tatu

## Mahkama Nyenginezo

Kuanzishwa kwa Mahkama nyengine. *Kif. 32 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**100**. Baraza la Wawakilishi linaweza kuanzisha Mahkama nyengine zilizo chini ya Mahkama Kuu na bila kuathiri masharti ya Katiba hii, Mahkama hizo zilizoainishwa zitakuwa na uwezo na madaraka ya aina ambayo yataainishwa katika Sheria.

## Sehemu ya Nne

### Utaratibu wa kupeleka Hati na kutekeleza maagizo yaliyomokatika Hati zilizotolewa na Mahkama

**101**.-(1) Hati zenye maagizo yaliyotolewa na Mahkama za Tanzania Bara na Mahkama za Zanzibar katika mashauri ya madai ya aina zote na mashauri ya jinai ya aina zote (pamoja na hati za kuamuru kukamatwa watu) zaweza kupelekwa mahali popote nchini Tanzania na maagizo hayo yaweza kutekelezwa mahali popote nchini Tanzania kwa kufuata masharti yafuatayo:

Utekelezaji wa maagizo ya Mahkama utafanywa nchini Tanzania kote.

(a) iwapo Mahkama imetoa hati yenye maagizo yatakayotekelezwa mahali ambapo Mahkama hiyo haina mamlaka; basi hati hiyo itapelekwa huko na maagizo yaliyomo katika hati hiyo yatatekelezwa kwa mujibu wa utaratibu unaotumika huko kwa ajili ya kupeleka hati au kutekeleza maagizo yaliyomo katika hati iliyotolewa na Mahkama yenye mamlaka huko ilikopelekwa hati; na

(b) iwapo sheria inayotumika huko ilikopelekwa hati imeweka masharti kwamba hati zilizotolewa na Mahkama ya mahali pengine ni lazima ithibitishwe kwanza na Mahkama yenye mamlaka mahali hapo inapotumika sheria hiyo basi kila hati iliyotolewa na Mahkama ya mahali pengine itabidi ithibitishwe kwanza kwa mujibu wa sheria hiyo kabla maagizo yaliyomo katika hati hiyo hayajatekelezwa.

(2) Iwapo mtu amekamatwa mahali popote nchini Tanzania kwa mujibu wa hati ya kuamuru kukamatwa kwake iliyotolewa na Mahkama ambayo haina mamlaka mahali hapo alipokamatwa mtu huyo, basi mtu atahesabiwa kuwa yuko chini ya ulinzi halali na anaweza kufikishwa mbele ya Mahkama iliyotoa hati hiyo, lakini masharti haya yaliyomo katika kifungu hiki itabidi yatumiwe bila kuathiri masharti ya sheria inayotumika hapo mahali alipokamatwa mtu huyo.

(3) Masharti yaliyomo katika kifungu hiki hayatazuia sheria kuweka utaratibu kwa ajili ya kupeleka nje ya Tanzania hati zilizotolewa na Mahkama za Tanzania Bara au Mahkama za Zanzibar.

## Sehemu ya Tano

## Tume ya Utumishi ya Mahkama

Tume ya Utumishi ya Mahkama.
*Kif. 56 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**102**.Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama ambayo muundo, kazi na uwezo wake utakuwa kama ilivyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

**102A.** [Kimefutwa].

**103.** [Kimefutwa].

# SURA YA SABA

## Sehemu ya Kwanza

## Fedha

### Masharti ya Fedha Yahusuyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**104**.-(1) Kutakuwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao bila ya kuathiri sheria nyengine yoyote inayotumika, zitawekwa fedha zote zitakazopatikana kutokana na njia mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa: Mfuko Mkuu wa Hazina na fedha nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

(a) kulipwa katika mfuko wa Serikali (mbali na ule mfuko wa Hazina) na ambao utawekwa kwa shughuli maalum; au

(b) kwa kuwekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Mabenki mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa madhumuni ya kulipa matumizi yoyote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ila ijulikane tu kwamba fedha hizo hazitotolewa kutoka mfuko huo mpaka iwe utolewaji wa fedha hizo umekubaliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au kwa sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni hayo.

**105**.-(1) Waziri anayehusika na Fedha atatayarisha makadirio ya matumizi kwa ajili ya Serikali kwa mwaka unaofuatia na atayapeleka Baraza la Wawakilishi. Makadirio.

(2) Makadirio ya matumizi yataonesha matumizi mbali mbali yanayohitajika kisheria (kama yalivyotafsiriwa katika

kijifungu cha (3) cha kifungu cha 106) na matumizi mengine ya kawaida ambayo yanahitajika kutolewa katika Mfuko wa Hazina.

**106**.-(1) Waziri anayehusika na mambo ya fedha atapeleka Baraza la Wawakilishi mapema iwezekanavyo, kila mwaka wa fedha unapoanza Mswada kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya Serikali ukiwa na kasma zinazohusika kwa shughuli mbali mbali zinazohitajika pamoja na jumla ya fedha zote zinazoombewa kwa matumizi hayo mbali na matumizi yanayohitajika kisheria kwa mwaka huo wa fedha.

Ruhusa ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina kwa Sheria ya Matumizi ya Fedha.

(2) Inapotokea:

(a) kwamba fedha zilizotumika au zinazotaka kutumika katika mwaka wowote wa fedha kwa madhumuni fulani ni zaidi ya fedha zilizoruhusiwa na Sheria ya Matumizi ya mwaka ule; na

(b) kwamba fedha zilizotumika au zinazotaka kutumika (mbali ya matumizi yanayohitajika kisheria) kwa mwaka wowote ule wa fedha kwa madhumuni yoyote yale na ambayo fedha hazikuidhinishwa katika Sheria ya Matumizi ya mwaka ule.

Maelezo ya matumizi ya ziada, au, kadri itavyokuwa Makadirio ya matumizi ya nyongeza yatawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi kuyakubali hayo Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza au Maelezo ya Matumizi ya Ziada, kutawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi Mswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinishwa matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, na fedha hizo zitatumiwa kulipia gharama za shughuli zinazohusika na Makadirio au Maelezo hayo.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki na vifungu vitavyofuata "Matumizi yanayohitajika kisheria" maana yake ni:

(a) matumizi yanayotoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina au katika Mapato ya Taifa kwa masharti ya vifungu vya sheria nyengine yoyote inayotumika;

(b) riba juu ya deni la Taifa, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni, na gharama zote ambazo zinaambatana na usimamizi wa deni hilo.

**107**.-(1) Hakuna malipo yatayofanywa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ila kwa idhini ya Waziri anayehusika na fedha kwa kutoa waraka maalum kuhusu matumizi hayo.

Malipo kwa idhini ya Hati Maalum.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 108 hakuna idhini itayotolewa ila kwa matumizi yaliyokubaliwa na Sheria ya Matumizi ya mwaka unaohusika au kwa maelezo ya ziada au kwa kadri itavyokuwa matumizi ya nyongeza yaliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kifungu cha 106(2) au kwa shughuli ambazo kisheria zinalipwa toka katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**108**.-(1) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga Sheria kwa kuanzisha Mfuko wa Matumizi ya Dharura na kwa kumruhusu Waziri anayeshughulikia mambo ya fedha, ikiwa ataridhika kwamba kumekuwa na jambo la dharura na muhimu linalohitaji matumizi na ambalo hakuna njia nyengine ya kisheria ya kupata matumizi hayo, kutoa fedha katika Mfuko huo kwa ajili hiyo.

Matumizi ya mfuko wa dharura.

(2) Pale ambapo fedha zimetolewa katika Mfuko huo, Matumizi ya Nyongeza yatapelekwa Baraza la Wawakilishi kwa

haraka inavyowezekana kwa madhumuni ya kuzirejesha fedha hizo zilizotumika.

Matumizi ya fedha kabla ya sheria kuanza kutumika.

**109**.-(1) Iwapo mwaka wa Fedha wa Serikali umeanza na Sheria ya Matumizi ya Fedha ya Serikali inayohusika na mwaka huo haijaanza kutumika basi Rais wa Zanzibar anaweza kuidhinisha fedha itolewe kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya kulipa gharama za lazima za shughuli za Serikali, na fedha hizo zitatumika kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu tangu mwanzo wa mwaka wa fedha au mpaka Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali itakapoanza kutumika kutegemea ni lipi kati ya mambo hayo litakalotokea mapema zaidi.

(2) Kwa sharti ya kwamba uidhinishaji huo kwa kipindi hicho hautozidi robo ya fedha ambazo ziliombwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kama zilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha mwaka wa fedha uliomalizika; lakini na vile vile kwa sharti ya kwamba fedha hizo kwa pamoja zitaingizwa katika vifungu vinavyohusika katika Sheria ya Matumizi ya Fedha inayofuata.

Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**110**.-(1) Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa kifungu hiki, deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar maana yake ni deni lenyewe na pia faida inayolipwa juu ya deni hilo, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni pole pole na gharama zile zinazoambatana na usimamizi wa deni hilo.

Malipo ya baadhi ya maafisa. *Kif. 36 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**111**.-(1) Watumishi wa Serikali wanaohusika na masharti ya kifungu hiki watalipwa mshahara na posho kama itavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Mishahara na marupurupu kwa watu wanaoshika nyadhifa zinazohusiana na kifungu hiki pamoja na malipo ya uzeeni na kiinua mgongo italipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

(3) Mishahara inayolipwa kwa watu wa aina hii (mbali na posho ambalo linazingatiwa katika pencheni) hautobadilishwa kwa madhumuni ya kumkandamiza baada ya kuteuliwa kwake.

(4) Inapokuwa mshahara wa mtu au masharti mengine ya utumishi yanategemea na kuchagua kwake, mshahara au masharti ambayo kwa madhumuni ya kijifungu cha (3) yatajaaliwa ni kwa manufaa yake zaidi kulikoni mshahara au masharti mengine aliyoyawacha.

(5) Kifungu hiki kinawahusu Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, Spika, Jaji Mkuu, Majaji wa Mahkama Kuu, Kadhi Mkuu, Wajumbe wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Tang. Nam. 47/2010.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**112**.-(1) Kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atakaeteuliwa na Rais.

(2) Mtu hatoweza kuchaguliwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mpaka awe na sifa zifuatazo:

(a) Shahada ya Chuo Kikuu inayotambulika inayohusiana na mambo ya Uchunguzi wa Hesabu; au

(b) Shahada nyenginezo za diploma za uchunguzi wa hesabu; na

(c) Mafunzo yanayohusiana na mambo hayo ambayo yamepatikana baada ya kupata moja kati ya shahada yoyote iliyoainishwa katika kijifungu cha

(2) (a) cha kifungu hiki na kwamba amefanya kazi katika shughuli hizo kwa muda usiopungua miaka mitano.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na jukumu juu ya mambo yafuatayo:

(a) kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe;

(b) kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi au fedha arnbazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

(c) angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kila mtumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar aliyeruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, kumbukumbu, hati za maelezo, taarifa na hati nyenginezo zote zinazohusika na hesabu za aina yoyote iliyotajwa katika kijifungu cha (3) cha kifungu hiki.

(5) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (3) (c) cha kifungu hiki. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kitachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasi1isha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi au Naibu Spika ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi.

(6) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa pia na jukumu la kutekeleza kazi na shughuli nyengine, na atakuwa na madaraka mengine ya namna mbali mbali, kama itakavyoelezwa na sheria, kuhusu hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au hesabu ya Mashirika na Makampuni ya Umma ya Zanzibar.

(7) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (3), (4) na (5) ya kifungu hiki, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwengine yeyote au Idara yoyote ya Serikali, lakini maelezo haya ya kifungu hiki hayataizuia Mahkama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mdhibiti

na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au siyo.

(8) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatoanza kazi yake ila kwanza ale Kiapo cha Uaminifu na kiapo chengine chochote kitachowekwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya utendaji wake wa kazi.

Kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**113**.-(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyengine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (3) cha kifungu hiki, venginevyo ataendelea na kazi hiyo hadi kutimiza umri wa kuacha kazi kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Iwapo suala la kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki linahitaji kuchunguzwa, basi utaratibu ufuatao ndio utakaotumika:

(a) Rais atateua Tume Maalum ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili;

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lote pamoja na ushauri wao kama huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyengine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(3) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (2) itamshauri Rais kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyengine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamuondoa kazini.

(4) Iwapo Tume itamshauri Rais kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali asiondolewe kazini basi Rais anaweza kukubali au kukataa mapendekezo hayo na hapo Rais atatumia busara zake.

(5) Mtu ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au aliyepata kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyengine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## Sehemu ya Pili

## Masharti ya Fedha Yahusuyo Mambo ya Muungano.

**114**. Fedha zote ambazo ni sehemu ya mchango wa Muungano na ambazo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inawajibika kulipa zitakuwa ni gharama itakayotoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Mchango wa Muungano.

**115**. Hakuna fedha itayotumiwa katika Sehemu hii hadi: Uwezo wa kutumia kasma.

(a) Tume ya Pamoja ya Fedha inayohusu mambo ya Muungano kama ilivyoanzishwa na Katiba ya Muungano imechambua mapato na matumizi ya shughuli za Muungano na kutoa mapendekezo yake kwa vyombo vinavyohusika juu ya mgawanyo wa matumizi hayo; na

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuyakubali mapendekezo hayo na mgawanyo wake.

## SURA YA NANE
## Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Kamisheni ya Utumishi wa Umma. *Kif.58 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**116.**-(1) Kutakuwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi, chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya utumishi wa umma kwa Zanzibar.

(2) Muundo, kazi na uwezo wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma itakuwa kama itakavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Tume ya Utumishi ya Serikali. *Kif.59 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**117.** Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Serikali kama itavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Uwezo wa Tume za Utumishi. *Kif.60 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**118**. Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Tume za Utumishi zilizotajwa ndani ya Katiba zitakuwa na mamlaka yafuatayo:

(a) kuajiri watu kushika nafasi za utumishi;

(b) kuthibitisha ajira zao za utumishi;

(c) kusitisha au kuachisha utumishi wao;

(d) kupendekeza serikalini mishahara na marupurupu ya watumishi wao; na

(e) mamlaka mengine yoyote zitakazopewa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

## SURA YA TISA

### Tume ya Uchaguzi

Tume ya Uchaguzi. *Kif. 37 cha Sheria Nam. 2/2002 na Kif. 4 cha Sheria Nam 8/2002.*

**119**.-(1) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais kwa utaratibu atakaoona unafaa;

(b) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kufuatana na mapendekezo ya Kiongozi wa shughuli za Serikali kwenye Baraza la Wawakilishi;

(c) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kufuatana na mapendekezo ya Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi au iwapo hakuna kiongozi wa upinzani basi kwa kushauriana na vyama vya siasa;

(d) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu;

(e) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kama Rais atakavyoona inafaa.

(2) (a) Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi atakuwa mtu aliyekuwa au mwenye sifa za kuwa Jaji katika Mahkama Kuu au Mahkama ya Rufaa katika nchi yoyote iliyo mwanachama wa Jumuiya ya Madola au mtu anayeheshimika katika jamii.

(b) Tume ya Uchaguzi itamteua Makamo Mwenyekiti kutoka miongoni mwa Wajumbe wake.

(3) Watu wafuatao hawataweza kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi yaani:

(a) Waziri au Naibu Waziri;

(b) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au ikiwa ni miongoni mwa majeshi ya Tanzania au ana wadhifa wowote ambao kisheria haruhusiki kuwa mjumbe wa Tume;

(c) Mbunge au mtu mwengine mwenye madaraka ya aina yoyote yaliyotajwa na Sheria iliyotungwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) ya Ibara ya 67 ya Katiba ya Muungano;

(d) Kiongozi wa chama chochote cha Siasa.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengine ya kifungu hiki, Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi atasita tu kuwa Mjumbe litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) ukimalizika muda wa miaka mitano tangu alipoteuliwa; au

(b) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Mjumbe lingemfanya asiweze kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi.

(5) Rais anaweza tu kumuondoa katika madaraka Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake, ama kutokana na maradhi au sababu nyengine yoyote, au kwa sababu ya tabia mbaya au kupoteza sifa za kuwa Mjumbe.

(6) Mjumbe wa Tume ataondolewa kwenye madaraka yake na Rais ikiwa suala la kuondolewa kwake kwenye madaraka

limepelekwa kwa Tume maalum iliyoundwa kwa ajili hiyo chini ya kijifungu cha (7) na Tume hiyo imependekeza kwa Rais kwamba Mjumbe huyo angefaa aondolewe kutokana na kutomudu kazi zake kama ilivyoelezwa hapo juu.

(7) Ikiwa Rais atahisi kwamba suala la kumuondoa Mjumbe wa Tume lingefaa kuchunguzwa, basi:

(a) Rais atateuwa Tume Maalum itayokuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wasiopungua wawili kutokana na watu wanaoshikilia au waliowahi kushika wadhifa wa Jaji wa Mahkama zenye mamlaka ya kusikiliza kesi za aina zote Tanzania, au Jaji wa Mahkama ya Rufaa yenye mamlaka ya rufaa kutoka Mahkama hizo; na

(b) Tume itachunguza suala hilo na itapendekeza kwa Rais kama Mjumbe huyo angefaa aondolewe au la.

(8) Ikiwa suala la kumuondoa Mjumbe limepelekwa kwa Tume Maalum kwa kuchunguzwa, Rais anaweza kumsimamisha kazi Mjumbe huyo na kumsimamisha huko kunaweza wakati wowote kukatenguliwa na Rais, na kwa hali yoyote hakutokuwa na taathira yoyote ikiwa Tume hiyo imependekeza kwamba Mjumbe huyo asiondolewe kwenye madaraka yake.

(9) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni Idara inayojitegemea na mtendaji mkuu wake atakuwa ni Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye atateuliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa masharti ya sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(10) Kiwango cha mikutano ya Tume ya Uchaguzi ni Mwenyekiti au Makamo Mwenyekiti na Wajumbe wanne na kila uamuzi wa Tume ni lazima uungwe mkono na Wajumbe walio wengi.

(11) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kuwateuwa Wajumbe wa kusimamia uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani na bila ya kuathiri masharti ya sheria kama hiyo au maagizo ya Tume ya Uchaguzi, madaraka ya Tume ya Uchaguzi ya kusimamia uchaguzi yanaweza kutekelezwa na Wajumbe hao.

(12) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali, au maoni ya chama cha siasa.

(13) Hakuna Mahkama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(14) Katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano.

Majimbo.
*Kif. 61 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**120**.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, Zanzibar inaweza kugaiwa katika majimbo ya uchaguzi yenye majina na mipaka kama yatakavyoelezwa na Tume.

(2) Baraza la Wawakilishi linaweza kuweka kisheria, idadi ndogo kabisa ya majimbo ya uchaguzi yasiopungua 40 na idadi kubwa kabisa ya majimbo yasiozidi 55.

(3) Majimbo yote yatakuwa karibuni na wakazi sawa sawa kama itakavyoonekana na Tume, lakini Tume inaweza kuepuka shuruti hii kwa kiwango kile kinachofikiria kuwa inafaa kwa ajili ya kuzingatia:

(a) idadi ya watu na zaidi katika kuhakikisha uwakilishi unaofaa katika miji mikubwa na miji ya mashamba yenye idadi ndogo ya watu;

(b) ukuaji wa idadi ya watu;

(c) njia za usafiri;

(d) mipaka ya sehemu ya utawala, na kwa madhumuni ya kifungu hiki idadi ya wakaazi wa sehemu yoyote ya Zanzibar itahakikishwa na ripoti ya kuhesabu watu ya karibuni sana ambayo imefanywa kwa mujibu wa sheria.

(4) Katika kipindi cha miaka 8 hadi 10 au wakati wowote Tume itachunguza idadi ya mipaka na majina ya majimbo hayo kwa kiwango kile ambacho inahisi ni wajibu kuangaliwa upya, na inaweza kwa kutoa tangazo, kubadili idadi, mipaka na majina ya majimbo hayo.

(5) Iwapo hesabu ya idadi ya watu imeshafanywa kwa mujibu wa sheria, au iwapo mabadiliko yamefanywa katika mipaka ya sehemu yoyote ya utawala, Tume inaweza ikachunguza suala hilo na kuweka mabadiliko hayo katika kiwango kile ambacho Tume inahisi ingefaa kufanyiwa mabadiliko hayo.

(6) Amri yoyote iliyofanywa na Tume chini ya kifungu hiki itatangazwa katika Gazeti Rasmi na itaanza kutumika tarehe ambayo itaainishwa katika Gazeti hilo.

## SURA YA KUMI
## Idara Maalum

**121**.-(1) Kutakuwa na ldara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kazi zake na shughuli zake zitakuwa kama zitavyoainishwa katika sheria zinazohusika.

ldara Maalum. *Kif. 62 cha Sheria Nam. 9/2010.*

(2) Idara Maalum zilizoainishwa katika kijifungu cha (1) hapa juu ni:-

(a) Jeshi Ia Kujenga Uchumi (kwa ufupi JKU);

(b) Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (kwa kifupi KMKM);

(c) Chuo cha Mafunzo (cha wahalifu).

(3) Rais wa Zanzibar anaweza, ikiwa ataona inafaa kuanzisha Idara nyengine yoyote kuwa Idara Maalum.

(4) Mtu yeyote aliye katika utumishi wa Idara Maalum haruhusiwi kujishughulisha na mambo ya siasa, isipokuwa kupiga kura katika uchaguzi wowote kulingana na masharti ya kifungu cha 7 cha Katiba.

Tume ya Utumishi ya Idara Maalum.
*Kif. 63 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**122**. Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya ldara Maalum ambayo uwezo wake, nguvu zake, kazi zake na Kanuni za mwenendo wake zitakuwa kama zitavyoainishwa katika sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo.

Uwezo wa Rais katika Idara Maalum.

**123**.(1) Rais atakuwa Kamanda Mkuu wa Idara Maalum na atakuwa na uwezo wa kufanya chochote kile anachohisi, kwa maslahi ya Taifa, kinafaa.

(2) Uwezo wa Rais chini ya kijifungu cha (1) unaingiza uwezo wa kutoa amri ya kufanya shughuli yoyote inayohusiana na Idara hiyo kwa manufaa ya Taifa.

## SURA YA KUMI NA MOJA
## Mamlaka ya Baadhi ya Vyombo vya Muungano

**124**.-(1) Vyombo vilivyoainishwa chini ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki na kama vilivyoanzishwa kwa mujibu wa vifungu vya Katiba ya Muungano, vitakuwa na mamlaka ya kutekeleza shughuli zake Zanzibar kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa katika Katiba ya Muungano na Sheria yoyote nyengine iliyotungwa na ama Bunge au Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo.

Mamlaka ya baadhi ya vyombo vya Muungano kutumika Zanzibar.
*Kif. 64 cha Sheria Nam. 9/2010*

(2) Vyombo vyenyewe vilivyotajwa katika kijifungu cha (1) ni:

(a) Mahkama ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano;

(b) Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano;

(c) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, vyombo vilivyoainishwa katika kijifungu cha (2) vitahesabika kama ni vyombo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika shughuli zake hapa Zanzibar.

## SURA YA KUMI NA MBILI
## Vyombo Vyengine vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

### Sehemu ya Kwanza
### Tume ya Mipango

**125**.-(1) Kutakuwa na Tume ya Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ndio chombo cha juu chenye uwezo wa kupanga na kusimamia utekelezaji wa maendeleo ya kiuchumi na mipango ya huduma za jamii katika Zanzibar.

Tume ya Mipango.

(2) Taratibu za utekelezaji wa kazi na majukumu ya Tume ya Mipango pamoja na wajumbe wa Tume utakuwa kama itavyoelezwa katika Sheria itayotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Wajumbe wa Tume.

**126**. Wajumbe wa Tume ya mipango na utaratibu wa mikutano utakuwa kwa mujibu wa Sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Katibu wa Tume ya Mipango.

**127**. Kutakuwa na Katibu wa Tume ya Mipango ambaye atateuliwa na Rais.

## Sehemu ya Pili

## Serikali za Mitaa

Serikali za Mitaa. *Kif. 65 cha Sheria Nam. 9/2010.*

**128**. Kutakuwa na Serikali za Mitaa ambazo uchaguzi wa viongozi wake, madaraka na kazi za kila Serikali ya Mtaa zitakuwa kama zitavyoelezwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

## SURA YA KUMI NA TATU

## Mambo ya Jumla

Kujiuzulu. *Kif. 66 cha Sheria Nam. 9/2010*

**129**.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, mtu yeyote ambaye ametajwa, amechaguliwa au ameteuliwa kushika wadhifa wowote ule ulioainishwa na Katiba hii, anaweza kujiuzulu kutoka katika wadhifa huo kwa maandishi aliyoweka saini yake akiyapeleka kwa mtu aliyemtaja, aliyemchagua au aliyemteua.

(2) Mtu aliyetoa taarifa ya kujiuzulu kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, atahesabiwa kuwa amejiuzulu tangu siku ile ambayo taarifa yake ya kujiuzulu

itakapopokelewa na mtu yeyote aliyeruhusiwa kupokea taarifa hiyo na mtu anaehusika na kikao kinachohusika, lakini kama taarifa hiyo ya kujiuzulu imeeleza kwamba atajiuzulu siku za baadae mtu huyo atahesabiwa kuwa amejiuzulu tangu siku hiyo nyengine ya baadaye.

(3) Taarifa ya kujiuzulu kwa Rais itapelekwa kwa Spika ambaye ataiwasilisha kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(4) Taarifa ya kujiuzulu kwa Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri na Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi itapelekwa kwa Rais.

(5) Taarifa ya kujiuzulu kwa Spika, itapelekwa Baraza la Wawakilishi.

(6) Taarifa ya kujiuzulu kwa Naibu Spika, au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi itapelekwa kwa Spika.

Uteuzi mpya na kuarifiwa kuachishwa kazi.

**130**.(1) Iwapo mtu yoyote mwenye dhamana ya kazi yeyote iliyoanzishwa na Katiba hii amejiuzulu, basi ikiwa anazo sifa zote zinazohitajika na kwa kila hali anastahili, anaweza kuteuliwa au kuchaguliwa tena kushika madaraka ya kazi hiyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(2) Iwapo mtu ameachishwa kazi au amesimamishwa kazi itabidi chombo hicho au mtu huyo aliyemuachisha au aliyemsimamisha kazi amueleze kwa maandishi kwamba amemuachisha au amemsimamisha kazi.

Maelezo kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika Utumishi wa Serikali.

**131**. Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba hii kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ifahamike kuwa mtu yeyote mwenye mamlaka kwa mujibu wa Katiba hii, ya kumteua

au kumchagua mtu mwengine kushika madaraka ya kazi fulani anao pia uwezo wa kumteua au kumchagua Naibu au mtu ambaye atashika kwa muda na kutekeleza madaraka ya kazi hiyo.

Sheria za Muungano.

**132**.-(1) Hakuna sheria yoyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe ni kwa ajili ya mambo ya Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Sheria kama hiyo lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika.

(3) Pale sheria ndogo inapoundwa kwa mujibu wa uwezo uliowekwa chini ya kijifungu cha (1) na cha (2) cha kifungu hiki itatumika tu pale itakapotimiza shuruti zote zilizowekwa kwa matumizi ya Sheria Mama kama ilivyoainishwa katika kifungu hiki.

Masharti ya kutoza kodi.

**133**.-(1) Hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa sheria i1iyotugwa na Baraza la Wawakilishi au kwa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Masharti yaliyomo katika kijifungu cha (1) cha kifungu hiki hayatalizuia Bunge kutumia mamlaka yake ya kutoza kodi ya aina yoyote inayohusiana na mambo ya Muungano kwa mujibu wa madaraka ya Bunge hilo kwa kujua kwamba mashauriano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano yamefanywa na kukubalika sehemu zote mbili kabla kupitishwa sheria.

**134**.-(1) Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yanahitaji vyenginevyo:

Ufafanuzi. *Kif. 38 cha Sheria Nam. 2/2002 na Kif. 67 cha Sheria Nam. 9/2010.*

"Baraza la Mapinduzi" linajumuisha na Baraza la Mawaziri;

"Chama" maana yake ni chama cha siasa kilichosajiliwa rasmi chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya 1992;

"Jaji" maana yake ni Jaji wa Mahkama Kuu na inajumuisha Kaimu Jaji;

"Kiapo cha uaminifu" maana yake ni kiapo chochote cha uaminifu kama kitavyoainishwa na Baraza la Wawakilishi;

'Kiapo" kinajumuisha na uthibitisho;

"Kikao cha Baraza la Wawakilishi" maana yake ni kikao cha siku moja au sehemu ya siku endapo Baraza halikukaa kwa siku nzima kinachoanza kwa kusomwa dua na kumalizika kwa kuakhirishwa hadi siku inayofuata au siku nyengine ya baadae;

"Mfanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" maana yake ni mtu anayefanyakazi au anayeshikilia wadhifa wa kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Mashirika yake;

"Mkutano wa Baraza la Wawakilishi" maana yake ni mfululizo wa vikao vya Baraza kuanzia kikao cha kwanza hadi kufikia wakati ambao shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya mkutano huo zitakuwa zinamalizika;

"Mwaka wa Fedha" maana yake ni kipindi cha miezi 12 kinachomalizikia tarehe 30 Juni ya mwaka wowote au kwa siku nyengine yoyote kama Baraza la Wawakilishi litakavyoainisha kwenye Sheria;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Waziri" maana yake ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi aliyekabidhiwa wadhifa wa kazi ya Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

"Utumishi wa Umma" maana yake ni ajira katika utumishi unaosimamiwa moja kwa moja na Tume ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi ya Mahkama, Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na inajumuisha utumishi katika taasisi zinazojitegemea ambazo zinafanya kazi za Serikali au zinazomilikiwa na Serikali na kadri tafsiri itavyohitaji, inajumuisha utumishi katika Mashirika ya kibiashara yanayomilikiwa na Serikali. Isipokuwa kwamba haitajumuisha utumishi wa kisiasa na utumishi wa maofisa ambao Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa masharti ya wazi imewaondoa katika tafsiri ya Utumishi wa Umma.

(2) Ila iwapo maelezo yatahitaji vyenginevyo, uwezo wowote uliopewa Baraza la Wawakilishi na Katiba hii kwa kuanzisha au kuelezea jambo lolote basi utafanywa kwa kutungiwa sheria.

(3) Kwa madhumuni ya Katiba hii, mtu hatahesabiwa kuwa na madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu tu kwamba anapokea malipo ya uzeeni au malipo mengine ya aina hiyo kwa ajili ya utumishi wake wa zamani.

(4) Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yatahitaji vyengine, kila anapotajwa mtu mwenye dhamana ya kazi fulani kwa kutaja madaraka ya kazi yake, ifahamike kuwa mtu anayehusika kuwa ni pamoja na mtu yeyote ambaye ni Kaimu au aliyeteuliwa kwa njia ya halali kushikilia dhamana ya kazi hiyo.

(5) Iwapo Katiba inatoa uwezo au nguvu fulani, basi uwezo huo au nguvu hizo zinaweza kutekelezwa wakati wowote inapohitajika.

(6) Katika Katiba hii, kila yalipotajwa mamlaka ya kumwondoa mtu katika madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ifahamike kuwa mamlaka yanayohusika ni pamoja na mamlaka yaliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya sheria yoyote yanayomtaka mtu huyo au yanayomruhusu mtu huyo kustaafu.

(7) Iwapo mtu ameteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, kuwa Naibu au kushikilia madaraka ya kazi fulani wakati mtu maalum aliyeteuliwa kushika madaraka ya kazi hiyo anashindwa kutekeleza shughuli zinazohusika na kazi hiyo, basi haitaruhusiwa kufanya uchunguzi wowote, kutoa hoja yoyote juu ya uteuzi wa huyo Naibu kwa sababu tu kwamba huyo mtu maalum aliyeteuliwa kushika madaraka ya kazi hiyo hakushindwa kutekeleza shughuli zinazohusika na kazi hiyo.

(8) Katika kifungu chochote cha Katiba hii kinachosema kwamba hakuna mtu au chombo fulani kitachoingiliana na mtu au chombo chochote katika kutekeleza kazi zake basi hakitokuwa na maana ya kwamba Mahkama zitazuilika katika mamlaka yake katika suala lolote hata kama mtu huyo au chombo hicho kimetekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyengine yoyote.

(9) Katika Katiba hii, kila ilipotajwa sheria ambayo inabadilisha au kufuta sheria nyengine, ifahamike kuwa sheria inayohusika ni pamoja na sheria ambayo inarekebisha sheria hiyo nyengine au ambayo inaendeleza kutumika kwa hiyo sheria nyengine ama bila ya mabadiliko au baada ya kubadilishwa au kurekebishwa au sheria ambayo inaweka masharti mapya katika sheria nyengine.

Kufutwa Katiba ya 1979. *Kif. 39 cha Sheria Nam. 2/2002.*

**134A**. Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 1979 imefutwa.

Jina la Katiba na tarehe ya kuanza kutumika.

**135**.-(1) Jina la Katiba hii litakuwa “Katiba ya Zanzibar ya 1984”.

(2) Katiba hii itaanza kutumika kuanzia tarehe 12 Januari, 1985.